ISSN 2820-2686 | Toleo Na. 3 | Octoba - Machi 2022

# JARIDA LA WAKILI MKUU



**GABRIEL MALATA**
**WAKILI MKUU WA SERIKALI**



**HONGERA**

**MWAKA MMOJA WA MHE. RAIS SAMIA MADARAKANI**

osgtanzania osg_tanzania Email: info@osg.go.tz www.osg.go.tz

# BODI YA UHARIRI


## Mwenyekiti

**Dkt. Boniphace Nalija Luhende**

(Naibu Wakili Mkuu wa Serikali)

## Mhariri Mkuu

**Innocent P.M. Mungy**

(Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano)

## Mhariri wa Habari

**Sarah Obby Mwakyusa**

(Afisa Habari Mwandamizi)

## Mhariri wa Habari

**Dennis Julius Buyekwa**

(Afisa Habari)

## Msanifu wa Jarida

**Nyamhoni Robert Chacha**

(Afisa TEHAMA)

## Wajumbe

**George Nathaniel Mandepo**

(Mkurugenzi wa Usuluhishi)

**Abubakar Amin Mrisha**

(Mkurugenzi Msaidizi - Usimamizi wa Mashauri)

**Kiuye Mbwana Shemakame**

(Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti)

# Tahariri ya Mhariri



## Heko Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan Kwa Mwaka Mmoja wa Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita

**Innocent P.M. Mungy**

**Mhariri Mkuu**

Wakati tunaadhimisha mwaka mmoja wa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali linawapongeza watumishi wa OWMS kwa mafanikio makubwa ambayo wamechangia kwa Serikali ya Awamu ya Sita.

Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali linatoa pongezi kwa Menejimenti na Watumishi wote kwa kazi nzuri waliofanya katika kutekeleza wajibu wake kwa Serikali na Taasisi zake. Tumetoa mchango mkubwa sana katika kufanikisha malengo ya Serikali.

Chini ya viongozi wetu wakuu, Mheshimiwa Gabriel Pascal Malata na Dkt. Boniphace Nalija Luhende, OWMS imeweza kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri yote ya Madai na Usuluhishi yaliyofunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali na Taasisi zake ndani na nje ya Nchi.Tulifanikiwa pia kuingilia kati na kuendesha mashauri yanayozihusu taasisi binafsi ambazo Serikali ina maslahi au kugusa mali za Umma kama inavyoonekana kwenye makala ya mafanikio ya OWMS ndani ya Jarida hili.

Mafanikio tuliyoyapata yanatokana na Serikali ya awamu ya Sita kutuwezesha kwa hali na mali kufanya kazi yetu vizuri kwa kutupatia bajeti na maelekezo yaliyoiwezesha OWMS kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Tunampongeza kwa dhati kabisa Rais wetu mpendwa kwa mafanikio makubwa aliyopata katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wake. Jarida la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali linamtakia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan mafanikio zaidi katika kuliongoza Taifa letu Tanzania kwa ufanisi zaidi na kuyaboresha Maisha ya Watanzania. Mungu ambariki na kumpa afya njema na Maisha marefu.

Kazi inaendelea.

# Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri



**Dkt. Boniphace Luhende**
**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

Toleo la tatu la Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali ni maalumu kwa ajili ya kuadhimisha mwaka mmoja tangu kuingia madarakani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Katika kipindi hiki cha mwaka mmoja, watanzania wote tumeshuhudia mabadiliko na mafaniko makubwa.

Na sisi Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali tumekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha tunaiwakilisha vyema na kwa weledi mkubwa Serikali katika uratibu, usimamizi na uendeshaji, wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi yaliyofunguliwa na au dhidi ya Serikali na Taasisi zake.

Kwa kuzingatia majukumu ya Ofisi yetu, toleo hili litajumuisha matukio yote muhimu yaliyofanyika katika kipindi cha mwaka mmoja tangu ya kuingia Madarakani kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Matukio hayo yatagusa mafanikio katika uendeshaji wa mashauri na mafanikio ya kiutawala na kiutendaji tuliyopata kwenye kipindi hiki.

Miongoni mwa mafanikio makubwa tuliyopata ni kupata kibali cha kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Tayari tumepata mchoro pamoja na makadirio ya gharama za ujenzi (BOQ) wa Jengo la Ofisi Makao Makuu Dodoma ambapo kwa sasa Ofisi inaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha za ujenzi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. Katika kipindi hiki pia tumepata vitendea kazi ikiwemo ununuzi wa magari mapya 13, ajira mpya 26, kupandisha madaraja watumishi 59 na kufadhili mafunzo kwa watumishi ya muda mrefu na muda mfupi. Haya yote yamewezeshwa na awamu hii ya Sita na kwa hilo tunashukuru sana.

Mambo haya na mengine mengi yataakisiwa kwenye Jarida hili.

Naomba nimalizie kwa kuomba wasomaji wetu waendelee kutoa maoni kwa Bodi yetu ya Uhariri kwa ajili ya maboresho na maoni kuhusu Jarida hili. Kwa pamoja tutaweza kulifanya Jarida kutoa mchango chanya katika ukuaji wa sekta ya Sheria hapa nchini.

Nawatakia usomaji mwema wa toleo hili maalumu.

Asanteni.

# Yaliyomo:


06 Mafanikio ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Katika kipindi cha Mwaka Mmoja wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan

12 Serikali Mbioni Kuanzisha Mfumo wa Kupima Utendaji Kazi wa Mawakili

14 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu

18 Tanzania bado Inaheshimu na Kutekeleza Makubaliano ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

20 Waziri Simbachawene Atembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

22 Mheshimiwa Jaji Mkuu Azindua Juzuu za Taarifa ya Sheria

26 Tuishi Katika Falsafa ya Kuboresha Utendaji Katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

29 "Tuendelee Kufanya Kazi kwa Bidii" - Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

33 Jaji Mkuu Azindua Vitabu vya Mkusanyiko wa Mashauri ya Mahakama ya Kazi

37 Waziri Simbachawene Akutana na Viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

39 Ofisi ya Wakili Mkuu ya Serikali Yapongezwa Tanga


42 Shauri Dhidi ya Wakala wa Majengo Latupwa

44 Ofisi ya Wakili Mkuu Yashiriki Maadhimisho ya Kilele cha Siku ya Wanawake Duniani

47 Toeni Majalada – Mkuu wa Wilaya Ilala

51 Mahakama - Sio Kila Kesi ya Kikatiba Inaweza Kufikishwa Mahakamani

# Mafanikio ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Katika kipindi cha Mwaka Mmoja wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan






Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) ilianzishwa kupitia Amri ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotangazwa tarehe 13 Februari, 2018 (Tangazo la Serikali Na. 50 la Mwaka 2018). Amri hiyo ilitolewa na Mhe. Rais kwa mujibu wa Ibara ya 36 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977.

Aidha, Amri hiyo ilitolewa kufuatia Amri ya Rais iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 48 la Mwaka 2018 ya Marekebisho ya Muundo na Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, 2018. Amri hiyo Na. 48 ilianzisha Ofisi tatu ambazo ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 50 la Mwaka 2018, uanzishwaji wa OWMS ulilenga katika kuiwezesha Serikali kusimamia uendesha na uratibu wa karibu wa mashauri mbalimbali ya Madai na Usuluhishi ndani na nje ya nchi. Hii inajumuisha kuiwakilisha Serikali katika Mahakama zote za ndani na nje ya nchi na Mabaraza ya Usuluhihisi wa Migogoro ya Kitaifa na Kimataifa.

Lengo mahsusi la kuanzishwa kwa OWMS ilikuwa ni kuimarisha huduma za uwakili kwa Serikali na Taasisi zake. OWMS ilipewa jukumu la Uratibu, Usimamizi, Ushauri na Uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi kwa niaba ya Serikali na Taasisi zake ndani na nje ya Nchi.

## LENGO YA KUANZISHWA KWA OWMS

Lengo kuu la kuanzishwa kwa OWMS ni kuwa na Taasisi moja ya kiserikali inayowajibika na Uratibu, Usimamizi, Ushauri na Uendeshaji wa Mashauri yote ya Madai na Usuluhishi yanayofungulia na Serikali/Taasisi zake au dhidi ya Serikali/Taasisi zake ndani na nje ya Nchi. Malengo mengine ni pamoja na Kujenga taasisi yenye uwezo wa kitaalamu ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

## MAFANIKIO YA OWMS KATIKA KIPINDI CHA AWAMU YA SITA.

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, yamekuwepo mafanikio makubwa yaliyopatikana. Katika kipindi cha Utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita (Machi 2021 hadi Machi, 2022) Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliongezewa bajeti yake kutoka Shilingi Bilioni 11.48 kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 hadi Bilioni 12.13 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 5.4.

Kuongezeka kwa bajeti ya OWMS kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 katika kipindi

cha uongozi wa Awamu ya Sita, kumepelekea Ofisi kufanya shughuli zake kwa ufanisi na kupata mafanikio yafuatayo;-

### Kuiwakilisha Serikali Mahakamani na Mabaraza ya Usuluhishi

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kipindi cha mwaka mmoja wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan imeendesha mashauri ya Madai 1,102 na ya Usuluhishi 117. Hivyo kufanya jumla ya mashauri yaliyoendeshwa kwa kipindi cha mwaka mmoja kuwa 1,219. Aidha, Mashauri ya Madai yaliyomalizika hadi Januari 2022 na Serikali kushinda ni 444 na Mashauri ya Usuluhishi 6 na hivyo kuokoa kiasi cha Shilingi Bilioni 236.6.

### Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti wa Ubora

Katika kipindi cha Mwaka mmoja wa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya 6, OWMS imeimarisha mfumo wa kukusanya takwimu za kesi, kufanya ufuatiliaji wa mienendo ya kesi na kupitia sheria zinazohusu kesi za Madai na Usuluhishi. Pia Ofisi imeweza kuandaa Miongozo ya kusimamia na kudhibiti viwango vya ubora vya Mawakili katika uendeshaji wa kesi.Vile vile, Ofisi imeweza kuandaa Mkataba wa Huduma kwa Mteja ambao ni Serikali na Taasisi nzake.

### Mafunzo kwa Watumishi

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita, OWMS imewawezesha watumishi kupata mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kama ifuatavyo:-

- Mafunzo ya Shahada za Awali kwa watumishi watatu (3) na Shahada za Uzamili kwa watumishi tisa (9) na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 92 wa kada mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mawakili, Makatibu Sheria, Madereva, Makatibu Muhtasi na Wahudumu yalitolewa;
- Mafunzo kwa Viongozi (Menejimenti) ili kuweza kuwakumbusha mambo ambayo wanapaswa kuyafanya na kuyaishi kama viongozi;
- Mafunzo kwa Mawakili kuhusu masuala ya kesi za Usuluhishi;
- Mafunzo ya masuala yanayohusu Kesi za Madai kwa Mawakili takribani 500 kutoka OWMS, Wizara, TAMISEMI na Taasisi mbalimbali za Serikali kama vile NSSF, TPA, NHC, NIDA, EPZA, UDSM, OUT, TIB TCRA, TPDC na PSSSF.

### Ajira na Ujazaji wa Nafasi za Watumishi

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeweza kujaza nafasi mbalimbali za uongozi. Ofisi ilipata vibali vya kuajiri watumishi 23 wapya, Watumishi watatu (3) kwa nafasi ya ajira mbadala na mtumishi mmoja (1) wa kuhamia. Tayari Ofisi imeweza kujaza nafasi hizo na kufikia watumishi 159.

### Upandishwaji wa madaraja

Katika mwaka mmoja wa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweza kukamilisha zoezi la upandishaji wa madaraja kwa watumishi ambao walibainika kuwa na sifa kwa kuzingatia maelekezo

yaliyotolewa na Serikali ambapo Watumishi 59 wenye sifa walipandishwa madaraja na watumishi wawili (2) walibadilishwa kada kutoka usaidizi wa Kumbukumbu na kuwa Wakili wa Serikali Daraja la II baada ya kujiendeleza.

### Ununuzi wa Magari ya Ofisi

Katika kipindi cha mwaka mmoja, Ofisi imeweza kununua magari mapya 16 na kufanya Ofisi kuwa na jumla ya magari 31. Hii ilitokana na Serikali ya Awamu ya Sita kuipatia Ofisi fedha kulingana na mahitaji ya Bajeti kama ambavyo tuliombwa.

### Kuboresha Ushiriki wa Wadau na Uimarishwaji wa Taratibu pamoja na Miundombinu ya TEHAMA

Katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan, Ofisi imeweza kuandaa Mwongozo wa Mawasiliano ya OWMS na kuendelea kuboresha Tovuti ya Ofisi na kutoa majarida yanayoelezea shughuli za Ofisi ili kuitangaza Ofisi kwa wadau mbalimbali. Vilevile ofisi imeweza kununua vifaa vya mikutano kwa njia ya masafa ya video (Video Conference).

### Kufungua Ofisi za Mikoa

Ofisi imefungua Ofisi katika Mikoa yote 16 yenye Masijala za Mahakama Kuu.

### Kupunguza Maambukizi Mapya ya VVU, UKIMWI na Magonjwa yasiyoambukizwa na Kuboresha Huduma Kwa Waathirika.

Katika kutekeleza jukumu hili, Ofisi katika vipindi mbalimbali imeweza kuweka utaratibu na imekuwa inawakumbusha watumishi juu ya maambukizi ya VVU, UKIMWI na magojwa yasiyoambukizwa. Aidha, watumishi wameweza kupatiwa vifaa ya kujikinga na maambukizi ya VVU na UKIMWI.

### Kufanya Ukaguzi wa Ndani, Kuandaa Taarifa za Fedha, na Kuboresha Mifumo ya Usimamizi wa Fedha.

Ofisi imeweza kuandaa taarifa mbalimbali zikiwemo; Taarifa ya Fedha ya Mwaka 2020/2021, Taarifa ya Manunuzi ya Mwaka 2020/2021, Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2020/2021, Mpango Kazi wa Mwaka 2021/2022, Mpango wa Manunuzi wa Mwaka 2021/2022 na Daftari la Viashiria Hatarishi. Aidha OWMS imefanya maandalizi ya Daftari la Kumbukumbu la Mali za Ofisi, Kufanya ukaguzi wa ndani na kutoa ushauri juu ya usimamizi wa mifumo ya udhibiti wa ndani na matumizi sahihi ya rasilimali.

Ofisi imeweza kununua Kompyuta mpakato 68 na Kompyuta 35, hivyo kuwa na jumla ya Kompyuta mpakato 76 na kompyuta za mezani 146, seti mbili za vifaa vya kufanyia majadiliano na kuendesha Mashauri kimtandao tukiwa ofisini kwetu (Video Conference), Seva kwa ajili ya kuhifadhia taarifa mbalimbali za ofisi na vifaa mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi. Vile vile, Ofisi imelipa stahili viongozi na watumishi kwa mujibu wa Sheria, hivyo hakuna madeni.

### Kuimarisha Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa na kupunguza matukio yatokanayo na rushwa

Katika kufikia lengo hili katika Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Ofisi

imeendelea kuimarisha utekelezaji wa mkakati wa kupambana na rushwa kwa kupunguza matukio yatokanayo na rushwa kwa kutolewa elimu kwa watumishi juu ya madhara ya rushwa na athari zake kwa jamii.

### Ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya OWMS Dodoma

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kipindi cha Mwaka Mmoja wa Uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ofisi imeweza kuandaa na kupata mchoro, makadirio ya gharama za ujenzi (BOQ) wa Jengo la ofisi Makao Makuu Dodoma. OWMS imeweza pia kupata kibali cha kupatiwa fedha kutoka ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa sasa ofisi inaendelea kukamilisha maelekezo ya Wizara ya Fedha ili tuweze kupatiwa fedha za ujenzi huo unaoanza

### Ushiriki wa Watumishi Kwenye Maamuzi

Katika dhana nzima ya Utawala Bora, OWMS imeweza kuwashirikisha watumishi katika maamuzi kupitia vikao mbalimbali vya Idara, Baraza la Wafanyakazi na Mkutano wa Wafanyakazi wote.

### Kuwezesha Mifumo ya Udhibiti

Ofisi pia katika kipindi cha mwaka mmoja wa Uongozi wa Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassa Ofisi imeweza kuboresha Mifumo ya Udhibiti wa Ndani na Usimamizi wa Rasimali za Ofisi.

### Uandaaji wa Miongozo na Nyaraka za Uendeshaji wa Ofisi

Ofisi imeweza kuandaa miongozo na nyaraka mbalimbali za uendeshaji wa Ofisi ikiwa ni pamoja na Mwongozo wa Mawasiliano, matoleo mawili ya jarida la OWMS, Mwongozo wa matumizi ya Maktaba, Sera ya TEHAMA, Mwongozo wa Ukaguzi wa ndani, Mkataba wa Huduma kwa Mteja na Mwongozo wa uendeshaji wa Ofisi.

### Uandaaji wa Mpango Mkakati wa OWMS 2021/22 – 2025/2026

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, imeweza kuandaa Mpango Mkakati wa OWMS 2021/22 – 2025/26 na Rejista ya Viashiria Hatarishi vya OWMS.

### Kupatikana Hati Safi wa Hesabu za OWMS

Katika kipindi cha Uongozi wa Mwaka Mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ofisi imeweza kufunga vitabu vya hesabu kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 pamoja na kukamilisha ukaguzi wa vitabu hivyo kwa wakati. Aidha, ofisi imekuwa inapata hati safi katika kila mwaka tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018 hadi sasa.

### CHANGAMOTO

Pamoja na Mfanikio hayo ambayo OWMS imefanikiwa kuyapaya katika kipindi cha Mwaka mmoja wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ofisi pia ilikabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

1. Upungufu wa Watumishi 153 kwa mujibu wa Ikama iliyopo kwa sasa ambayo ina jumla ya Watumishi 312 lakini waliopo ni 159;

2. Maslahi kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili wa Serikali hayaendani na uzito wa majukumu ya Ofisi;
3. Ufinyu wa bajeti (Budget ceiling) na;
4. Kukosekana kwa Mawakili wenye stadi maalumu kwenye maeneo mtambuka (specilized skills).

## MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

Katika kukabiliana na changamoto kama zilivyoainishwa, Ofisi imendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo:-

1. Kuendelea kufanya majadiliano na Serikali ili kuomba kuongezewa wigo wa bajeti (ceiling) ili kuweza kutoa huduma stahiki na kuboresha mazingira ya kazi.
2. Kuomba Taasisi mbalimbali kuchangia katika kutatua baadhi ya changamoto;
3. Kuendelea kuwajengea uwezo Mawakili katika kuandaa utetezi na kuhakikisha kuwa tunawatumia Mawakili wa ndani kuendesha kesi zote za ndani na nje ya nchi pale ambapo sheria zinaruhusu kufanya hivyo.

## HITIMISHO

Katika kuendelea kuunga Mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kutekeleza jukumu la Kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri kwa ufanisi na weledi kwa niaba ya Serikali na Taasisi zake ili kuhakikisha Pato la Taifa na Uchumi wa Nchi unaongezeka kwa kutetea na kulinda maslahi ya Serikali ipasavyo kokote kule, iwe ndani ya nchi au nje ya nchi.



***Wakili Mkuu wa Serikali Gabriel Malata (kulia) na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt Boniphace Luhende.***



Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi
Mwanasheria Mkuu wa Serikali

# Serikali Mbioni Kuanzisha Mfumo wa Kupima Utendaji Kazi wa Mawakili

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, alisema kuwa Serikali ina mpango wa kuanzisha mfumo wa kupima utendaji wa Mawakili wake ili kuhakikisha wanafikia malengo waliyojiwekea.

Dkt. Feleshi amezungumza hayo alipotembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa lengo kuona wanavyotekeleza majukumu yao na kujitambulisha kwa Menejimenti na watumishi.

Dkt. Feleshi alisema kuwa mfumo huo wa kupima utendaji kazi kwa watumishi utaisaidia Serikali na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kujua utendaji kazi wa kila Wakili wa Serikali hatua itakayosaidia kuongeza kasi ya uendeshaji wa mashauri yanayoihusu Serikali na Taasisi zake

katika mahakama na vyombo vingine vya uamuzi yakiwepo Mabaraza ya usuluhishi.

“Mipango yetu ni kuwa na Taasisi Bora ya kisheria katika kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri yote ya Madai na Usuluhishi yanayoihusu Serikali ndani na nje ya nchi”, alisema Dkt. Feleshi.

Alisema, kupitia mfumo huo Serikali itapata nafasi nzuri ya kujua idadi na aina ya mashauri yanayoendeshwa na Wakili mmoja mmoja hivyo itasaidia kurahisisha ufuatiliaji wa mashauri kwa ukaribu, uendeshaji wa mashauri na kuhakikisha yanamalizika kwa wakati.

Aidha, amewataka Mawakili Waandamizi kuwasimamia na kuwajengea uwezo Mawakili wengine kwa lengo la kuhakikisha wanapata uzoefu wa kutosha ili waweze kusimamia vyema mashauri yote yanayoihisu Serikali.

Dkt. Feleshi amewasisitiza kuwa ni muhimu kwao kuendelea kuainisha changamoto mbalimbali wanazokutana nazo katika kusimamia na kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwani kwa kufanya hivyo itaisaidia Serikali kupiga hatua katika uendeshaji wa mashauri yake kwa ufanisi zaidi.

Amewasihi watumishi kuendelea kufanya kazi kwa juhudi amani na mshikamano huku akiahidi kuchukua changamoto zinazowakabili na kwenda kuzifanyia kazi kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufanyaji kazi kwa kila mtumishi na ofisi kwa ujumla.

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende, amemshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kufanya ziara ofisini hapo na kusema kuwa Ofisi imejifunza mengi na itakwenda kufanyia kazi ushauri uliotolewa ikiwepo



***Mwanasheria Mkuu wa Serikali Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (kushoto) na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt Boniphace Luhende wakielekea kuangalia shughuli zinazofanywa na Kitengo cha Masijala ya Sheria.***

kuweka mfumo mzuri wa kupima utendaji kazi wa watumishi wa ofisi hiyo.

“Ofisi imeshaanza maboresho na sasa tunajaribu kuweka mfumo wa kujua viwango vya utendaji kazi wa watumishi kwa mfano kuwa na mfumo wa kuweza kujua mashauri yaliyopo katika ofisi na kujua wangapi wapo ofisi na wangapi hawapo na wanafanya nini ingawa bado hatujafikia huko”. Dkt Luhende

Ziara hii ni ya kwanza kwa kiongozi huyo tangu ateuliwe kushika wadhifa huo na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan tarehe 12 Septemba 2021.



*Baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza mgeni rasmi katika maadhimisho ya ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yashiriki Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu

**Serikali imesema Maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu ni hatua iliyosaidia kuongeza mahusiano mazuri baina ya ofisi, na Wadau wake nchini kwa kuwa kusanyiko la Maadhimisho haya kwa pamoja linawakutanisha watoa huduma na wapokea huduma yaani Watumishi wa Umma na wananchi.**

Hayo yamesemwa na Mgeni Rasmi wa Maadhimisho ya mwaka 2022, Naibu Waziri Wizara ya Katiba na Sheria Mhe. Geofrey Mizengo Pinda alipokuwa akifungua maadhimisho katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam ambapo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ikiwa mdau muhimu wa masuala ya Maadili, Haki za Binadamu na Utawala bora ilishiriki.

Mhe Pinda alisema kuwa dhima ya Maadhimisho haya ni muhimu kwa ustawi wa jamii na nchi yetu kwa ujumla kwa kuwa kusanyiko la pamoja linawakutanisha watoa huduma na wapokea huduma yaani Watumishi wa Umma na wananchi.

Alisema utaratibu huu ni mzuri kwa kuwa unasaidia kuzileta pamoja pande mbili muhimu zinazo tegemeana yaani wananchi na Watumishi wa Umma katika kujenga Taifa letu kwa kusisitiza kuwa suala hili linatamkwa wazi katika Ibara ya 8 (1) ((b) na (d)) na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayozungumzia haki za jamii na lengo la Serikali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha ustawi wa wananchi kuwa Serikali inawajibika kwa wananchi na kwamba wananchi wana haki ya kushiriki katika shughuli za Serikali yao.

Alisema kuwa kufanya hivi kunaonyesha jinsi gani Serikali yetu inatambua umuhimu wa ushirikishwaji wa Umma katika masuala ya kitaifa ndio maana kusanyiko hili Pamoja na kujumuisha wananchi lakini pia limehudhuriwa na wawakilishi wa mataifa mbalimbali, Umoja wa Mataifa na sote tumesikia uzingatiaji wa Haki za Binadamu

katika nchi yetu kupitia hotuba mbalimbali zilizotolewa.

"Sina shaka kwa Viongozi na Wananchi tuliopo hapa sote kwa ujumla tutazingatia yote yaliyoambatana na matamko haya hivyo tutakuwa chachu ya kuimarisha Haki za binadamu na Mapambano dhidi ya Rushwa katika jamii". Alisema Mhe. Pinda.

Mheshimiwa Pinda alisema kuwa kwa kutambua umuhimu uliopo na kuzingatia uwezo wa haki hizi ndio sababu ilifikia uamuzi wa kuzifanya haki za Binadamu kuwa sehemu ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyoainishwa katika sehemu ya 3 ya Katiba kuanzia ibara ya 12 hadi 24, hivyo ni muhimu wananchi wote tukafahamu haki na wajibu wetu kwani hakuna haki bila wajibu.

"Wajibu wetu kama raia umefafanuliwa katika ibara ya 25 na 28 ya Katiba yetu hivyo ni vyema kila mmoja wetu akasoma na kuzingatia haya kwa ustawi wa taifa letu". Alisema Mhe. Pinda.

Aidha Mhe. Pinda alitumia Maadhimisho kuwaasa Watumishi wa Umma na Wananchi walioshiriki kuepuka vitendo vya rushwa na kuzingatia Haki za Binadamu katika kutoa huduma kwa Umma huku wakitambua kuwa wote tunatekeleza majukumu yetu kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 35 ya Katiba inayosema mtumishi akitoa na kupokea rushwa au akikiuka Haki za binadamu ni fedheha kwa Serikali hivyo mtumishi huyo hastahili kuendelea na utumishi wake.

Naibu Waziri alisistiza kuwa kila mwananchi kwa nafasi yake atekeleze wajibu wake kwa kutotoa wala kupokea rushwa kwani kutoa na kupokea rushwa yote ni makosa kwa kufanya hivyo itatusaidia sana kupunguza vitendo vya rushwa nchini.

Aliwataka wananchi hao kuwa mstari wa mbele kutoa Taarifa kuhusu vitendo vinavyohusiana na rushwa ili wote waweze kushiriki katika kutekeleza mkakati wa Taifa dhidi ya rushwa uliolenga kukomesha vitendo vya rushwa nchini

"Kama ambavyo mara nyingi tumemsikia Mhe. Rais wetu akizungumza kwa hisia sana



***Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Geofrey Mizengo (mwenye shati la bluu) akiteta jambo na Kamishna wa TAKUKURU ACP Salum Hamdun katika maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu***

dhidi ya vitendo vya rushwa nchini nawasihi wananchi wote tumuunge mkono Rais wetu Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa nguvu zetu zote kuhakikisha malengo ya kupambana na vitendo vya rushwa yanafikiwa" Mhe Pinda.

Aidha, Mhe Pinda amewataka wananchi kujikinga na ugonjwa wa UVIKO 19 kwa sababu ni janga ambalo halichagui nchi, mtu wala umri, hivyo amewaomba wananchi kuungana na Serikali katika kupambana na janga hilo kwa kuendelea kuwasikiliza wataalamu wa afya nchini pamoja na kuchukua tahadhari kwa kupata chanjo inayoendelea kutolewa nchi nzima.

Ametoa wito kuhusu wananchi kujitokeza kwenye zoezi la sensa linalotarajiwa kufanyika baadae mwaka huu. Amewasihi wananchi wote kujitokeza na kushiriki kikamilifu katika zoezi hilo kwa kuwa sensa ni zoezi muhimu sana kwa mipango endelevu ya Taifa letu, hivyo ameomba kila mwananchi amtaarifu mwenzake huku wote tukiwasikiliza viongozi na watoa elimu ikiwemo kujipatia taarifa sahihi kuhusu zoezi la sensa.

Naye Mwenyekiti wa Sekretariati ya Maadili na Haki za Binadamu Jaji wa Rufani Sivangilwa Mwangesi alisema kuwa umuhimu wa Maadhimisho haya ni kuendelea kuwakumbusha wananchi ushirikishwaji wa Umma katika masuala ya kitaifa

Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu kitaifa mwaka huu yalifanyika katika Viwanja vya Mnazi mmoja Jijini Dar es Salaam ambapo kauli mbiu ya maadhimisho ilikuwa ni "Zingatia Maadili, Piga Vita Rushwa, Heshimu Haki za Binadamu ili kuimarisha Utawala Bora".




***Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Geofrey Mizengo (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Taasisi mbambali katika maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu***

# Tanzania bado Inaheshimu na Kutekeleza Makubaliano ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

**Serikali ya Tanzania imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zinazolenga kutekeleza baadhi ya maamuzi ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR) kwa kutunga sera na sheria za kanuni zinazoendana na mahakama ya Afrika.**

Naibu Wakili Mkuu Dkt. Boniphace Luhende alisema hayo Jijini Dar es Salaam alipokuwa akiwasilisha uzoefu wake katika mkutano uliowakutanisha maofisa wa ngazi za juu wa Mahakama kutoka nchi mbalimbali za Afrika kujadili utekelezaji wa maamuzi ya Mahakama.

Dkt. Luhende aliwaambia washiriki wa Mkutano huo kuwa pamoja na kwamba Mwaka 2019 Tanzania iliondoa Azimio lake chini ya kifungu cha 34(6) cha Itifaki ya Mkataba wa Mahakama ya Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kinachowaruhusu watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali kuishtaki katika Mahakama hiyo, bado ina idadi kubwa ya kesi katika Mahakama na kujiondoa kwake hakujaathiri kesi zinazoendelea.

Alisema kwamba licha ya kujitoa, Tanzania bado inashikamana na Mahakama ya Afrika ambapo Tanzania inafungwa na Kifungu cha 30 cha Itifaki ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ambayo inaweka wajibu wa Utekelezaji wa hukumu za Mahakama.

Dkt. Luhende alisema kuna maombi karibu 156 dhidi ya Tanzani katika Mahakama ya Afrika  na sababu hiyo Tanzania inakabiliwa na




**Dkt. Boniphace N. Luhende**
**Naibu Wakili  Mkuu wa Serikali**

maamuzi kadhaa ya Mahakama ambayo yanaweza kuhitaji utekelezaji katika mfumo wetu wa ndani.

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali alieleza kuwa moja ya changamoto inayoikabili Tanzania katika utekelezaji wa uamuzi wa mahakama, ni pamoja na kutokuwepo kwa taratibu mahususi za utekelezaji wa hukumu za Mahakama ya Afrika , nchini.

"Hata katika kukosekana kwa taratibu za utekelezaji, Tanzania imechukua hatua mbalimbali kutekeleza baadhi ya maamuzi ya Mahakama ya Afrika kwa kutunga kanuni, sera na sheria. Moja ya mifano bora ya utekelezaji huo ni kutunga Sheria ya Msaada wa Kisheria namba 1 ya mwaka 2017" alisema Dkt. Luhende.

Alisema sheria hiyo ilitungwa ili kutoa msaada na kuratibu masharti ya huduma ya msaada wa kisheria kwa watu wasiojiweza. Alisema kabla ya kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria, huduma hizo zilikuwa kwa watu wanaokabiliwa na makosa Makubwa (Capital Offences) kama mauaji na uhaini.

Dkt. Luhende alisema kuwa katika Maombi Namba 027 ya mwaka 2015 kati ya Minani Evarist na Mohamed Abubakar dhidi ya Tanzania, ilibainika kuwa ni ukiukwaji wa haki ya kusikilizwa kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 7(1)(c) cha Mkataba wa Afrika kwa kushindwa kutoa msaada wa bure wa kisheria.

"Kwa maoni yetu kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria kumetokana na maamuzi ya Mahakama ya Afrika. Kwa kupitishwa kwa sheria, wigo wa matumizi ya msaada huo umepanuliwa kwa kesi zote za jinai na madai na kujumuisha vifungu mahususi kwa watoto walio katika mgogoro na sheria' Alisema.

Kupitia watoa Msaada wa Kisheria walioidhinishwa, mtu asiyejiweza ambaye ameshtakiwa kwa jinai anaweza kupewa msaada wa kisheria kwa kufuata utekelezaji wa uamuzi wa usaidizi wa kisheria kwa wale wanaohitaji katika kila kosa la jinai.


Naibu Wakili Mkuu pia alitaja hatua nyingine iliyochukuliwa na Serikali kuwa ni kuanzishwa kwa taratibu za makubaliano katika mashauri ya jinai kupitia marekebisho ya kifungu cha 194 A cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura. 20, [R.E 2019] ili kuongeza kasi ya mashauri na kupunguza idadi ya kesi zinazoendelea.

Serikali, kwa nia ya kuongeza kasi ya usikilizwaji na kupunguza mlundikano wa kesi, ilianzisha mashauriano katika Kifungu cha 194A cha Sheria ya Mwenendo Alisema vifungu kama hivyo vinaeleza kwamba wahusika katika kesi wanaweza kuingia katika makubaliano ya kujadiliana ambayo yanaweza kusababisha, kuondolewa kwa mashtaka Mtuhumiwa kwa kulipa fidia. Mpango huu unawiana na falsafa ya Mahakama ya Afrika inayosisitiza haja ya kuharakisha kesi za jinai.

Dkt. Luhende aliendelea kusema kuwa Serikali pia imeanzisha Huduma za Mahakama inayotembea (Mobile Court Services) kwa madhumuni ya kuleta huduma karibu na watu na kuimarisha upatikanaji wa Haki kwa wakati. Mahakama zinazotembea zinatumika kama Mahakama ya Mwanzo na Wilaya, tofauti pekee ni kuhamishika. Hatua hii inaendana zaidi na maamuzi ya Mahakama za Afrika zinazosisitiza kuwa haki inayocheleweshwa ni haki iliyonyimwa.

Alisema kuwa Serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha mifumo yake ya utoaji haki ya ndani na imeanza zoezi la uundaji shirikishi wa kuchambua mlolongo mzima katika usimamizi wa haki za jinai.

African Court on Human and Peoples' Rights



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. George Simbachawene akikagua Maktaba ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam*

# Waziri Simbachawene Atembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. George Simbachawene (Mb) ametembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa lengo la kujitambulisha kuona namna ambavyo Ofisi imekuwa ikitekeleza majukumu yake ya kila siku.

Akizungumza na viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mhe. Simbachawene amepongeza mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya muda mfupi tangu kuanzishwa kwake, ikiwa ni pamoja na kuokoa Kiasi kikubwa cha fedha ndani ya muda mfupi wa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya sita.

Mhe. Simbachawene ameahidi kushirikiana na viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kuwasemea watumishi wa Ofisi ili waweze kuboreshewa maslahi yao kwa kuzingatia ukweli kuwa kazi inayofanywa na watumishi ni kubwa na ya kizalendo hivyo inahitaji kupongezwa na kila mpenda maendeleo.

Mhe. Simbachawene ameongeza kuwa ameshangazwa na utendaji wa ofisi licha ya kuwa haina muda mrefu tangu kuanzishwa kwake lakini imefanya mambo makubwa ambayo yamevunja rekodi ya kiutendaji na kuwasihi watumishi wa OWMS kuendelea kufanya kazi kwa bidi.

Alisema amefurahishwa na taarifa iliyotolewa na Wakili Mkuu Serikali ya kuwa ndani ya muda mfupi Ofisi imefanikiwa kuokoa kiasi kikubwa cha fedha ambacho kitaisaidia Serikali katika kuendelea kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kwa manufaa makubwa ya taifa hili.

Mhe. Simbachawene alisema kuwa moja ya miradi ni bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere litakalokuwa na uwezo

wa kuzalisha megawati 2115, reli ya kisasa (SGR), vituo vya afya nchi nzima, daraja la Magufuli linalojengwa ziwa Victoria, pamoja miradi mbalimbali ya barabara itakayosaidia kuiunganisha nchi nzima kwa mtandao wa lami.

Mhe. Waziri ameipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu kwa uamuzi wake wa kutumia mifumo hasa katika uendeshaji na uratibu wa mashauri hatua ambayo imesaidia kuongeza ufanisi zaidi katika utekelezaji wa mashauri kote nchini.

"Yako mambo ambayo yamenivutia sana moja wapo ni mfumo wa uendeshaji na uratibu wa mashauri ya Serikali ndani ya ofisi hii, kwa kweli mfumo ule ni wazi, una kila aina ya sifa na kuwa mfumo wa hadhi ya kiwango cha mtetezi mkuu wa Serikali", alisema Mhe. Simbachawene.

Aidha Mhe. Waziri ameahidi kuendelea kuwekeza zaidi katika matumizi ya mifumo kwa Taasisi zilizoko chini yake kwa kuwa mifumo ile ndio itakayoenda kurahisha kuhakikisha tunafanya vizuri katika mashauri yote yanayoendeshwa na Serikali.

Akisoma taarifa ya Utekelezaji wa OWMS mbele ya Waziri wa Katiba na Sheria, Wakili Mkuu wa Serikali Gabriel Malata alisema kuwa ndani ya mwaka mmoja wa uongozi wa awamu ya sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan alisema kuwa Ofisi yake imefanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi Bilioni 236.6.

Ameeleza kuwa kiasi kilichookolewa ni fedha ambazo zingelipwa endapo Serikali ingeshindwa katika mashauri mbalimbali yaliyomalizika katika Mahakama ndani na nje ya nchi ambapo sasa fedha hizo zitaelekezwa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo nchini.

Mhe. Malata amemshukuru Mhe. Waziri kwa kutembeleza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali huku akimuahidi kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha hatua itakayosaidia kuiletea maendeleo nchi yetu.

Wakili Mkuu wa Serikali ameeleza kuwa jukumu kubwa la Ofisi yake ni Kuendesha, kusimamia na kuratibu Mashauri ya Madai na Usuluhishi yanayofunguliwa dhidi ya Serikali au Serikali katika Mahakama ndani na nje ya nchi ikiwamo kuingilia kati mashauri yanayofunguliwa dhidi ya Taasisi binafsi zenye maslahi ya Serikali.

Katika Ziara ya siku moja Mhe. Simbachawene aliongozana na Viongozi waandamizi wa Wizara, akiwemo Katibu Mkuu Wizara Katiba na Sheria Mary Makondo, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Khatibu Kazungu na Mkurugenzi Idara ya Haki za Binadamu Bi. Nkasori Sarakikya.



***Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. George B. Simbachawene (wa kwanza kushoto) akipokea maelezo ya Mkurugenzi Msaidizi Madai ya Ndani Deudatus Nyoni wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali***

# Mheshimiwa Jaji Mkuu Azindua Juzuu za Taarifa ya Sheria.



## Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma

### Jaji Mkuu wa Tanzania

Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma, amezindua Juzuu ya Taarifa ya Sheria za Tanzania kutoka Mwaka 2007 hadi 2020 zinazojumuisha maamuzi ya Mahakama Kuu Tanzania Bara na Visiwani pamoja na Mahakama ya Rufani.

Uzunduzi wa Juzuu hizo umeenda pamoja na uzinduzi wa Faharisi (Index) ya Sheria Mama na Sheria ndogo za kuanzia Mwaka 1961 mpaka mwaka 2020, vyote vikiwa katika mfumo wa nakala laini na ngumu, hatua ambayo imelenga kuwasaidia maafisa wa Mahakama na Wadau kutumia vitabu hivyo vya sheria katika kusimamia utoaji haki nchini.

Sambamba na tukio hilo Mhe. Jaji Mkuu amezindua

mfumo mpya wa kielektroniki kwa ajili ya kusajili, kutunza kumbukumbu na kuratibu leseni za Mawakili, (e-Wakili Management System) mara baada ya mfumo uliokuwa unatumika awali kuwa na changamoto kadhaa zilizopelekea zoezi hilo kutofanyika kwa ufanisi.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Jaji Mkuu Prof. Juma alisema kuwa hii ni mara ya tatu kwa machapisho kutolewa na Mahakama ya Tanzania ambapo Chapisho la kwanza lilikuwa kati mwaka 1980 hadi 1996 huku chapisho la pili lilikuwa kati ya mwaka 1997 hadi 2006. Alisema kuwa uamuzi wa mashauri mengi katika chapisho la tatu utaonekana kuwa ni wa Mahakama ya Rufani ikiwa ni muendelezo wa kutoa nakala nyingine za uamuzi wa Mahakama Kuu Tanzania bara na Visiwani kwa kila mwaka husika kuwa na chapisho la pili.

Prof. Juma alieleza kuwa machapisho ya mwanzo kabla ya uhuru yalianza Mwaka 1921 wakati Mahakama Kuu ya Tanganyika inaanza shughuli zake tarehe 3 Januari, 1921 ambapo maamuzi katika mashauri mengi kwa kipindi




***Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Profesa Ibrahim Hamisi (katikati) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Juzuu ya taarifa za Mahakama***

hicho yalitolewa taarifa kati ya mwaka 1921 mpaka 1952 ambayo yaliitwa (Tanganyika Territory Law Reports), hii ikiwa ni chapisho la kwanza.

Kwa mujibu wa Jaji Mkuu Prof. Ibrahimu Hamis Juma mwaka 1953 mpaka 1957 kulikuwa na chapisho la pili na baadae kuwa na chapisho la tatu mwaka 1958 mpaka 1966. Alisema kuwa katika mwaka 1967 mpaka mwaka 1972 machapisho ya makusanyiko ya uamuzi wa Mahakama Kuu yalitolewa (High Court Digests 1967 mpaka1972) na mwaka 1973 mpaka mwaka 1979 taarifa za juzuu zilitolewa (The Law Reports of Tanzania 1973-1979) kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mhe. Prof. Juma ameendelea kueleza kuwa baadae kuanzia mwaka 1980, Bodi ya Uhariri wa Juzuu ya Taarifa za Sheria ilibadilika na kuwa na uenyekiti kupitia Jaji wa Mahakama Kuu, Mhe. Barnabas Samatta na kuanzia kipindi hicho Mahakama ya Tanzania iliendelea na shughuli za uchapaji wa machapisho yote.

Aidha Mhe. Jaji Mkuu ametoa pongezi na shukrani za dhati kwa Serikali ya Tanzania chini ya uongozi wa Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan na Benki ya Dunia kwa kuendelea kutoa ufadhili kwa Mahakama ya Tanzania kwa kuwezesha na kufanikisha matoleo haya ya vitabu hivi vya kisheria kwa miaka yote hii na Faharisi za Sheria Mama na Sheria ndogo za kuanzia Mwaka 1961 mpaka 2020, vyote vikiwa katika mfumo wa nakala laini na nakala ngumu.

“hawa wamekuwa wadau




***Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania Mhe. Prof Ibrahimu Hamis Juma (katikati) akionyesha moja ya vitabu vya Juzuu za taarifa za sheria za Tanzania***

wakubwa wa utoaji haki katika mashauri ya ngazi zote za Mahakama na wamekuwa wanasaidia Mahakama ya Tanzania katika mambo mbalimbali yanayohusu utekelezaji wa utoaji haki," alisema Jaji Mkuu.

Jaji Mkuu ameahidi kuwa Mahakama itaendelea kuimarisha upatikanaji wa nakala za maamuzi kwa miaka ya nyuma kuanzia mwaka 1980 mpaka Mwaka 2006. Aidha ameomba Mahakama kupitia Idara ya Menejimenti ya Mashauri na Kitengo cha Maktaba kuendeleza utaratibu huo wa kuandaa Faharisi ya Sheria Mama na Sheria ndogo kuanzia mwaka 2021 na kuendelea.

Naye , Jaji kiongozi wa Mahakama ya Tanzania, Mhe, Mustapher Siyani ameeleza kuwa Juzuu za Taarifa yaa Sheria hizi ni nyenzo muhimu za kazi kwa kila mwanataaluma ya sheria nchini kwa kuwa kutokana na taarifa hizo maamuzi mbalimbali ya mashauri yanayoakisi msimamo wa sheria katika nchi yetu yatapatikana.

Vilevile mesema kuwa taarifa hizo zitawasaidia wananchi na Mawakili wanaofika mahakamani kila siku kutafuta haki kujua misimamo mbalimbali ya kisheria kupitia uamuzi ya Mahakama za juu.

Akizungumza katika hafla hiyo, Naibu Mratibu wa Bodi ya Uhariri wa Majuzuu ya Taarifa za Sheria Tanzania, Mhe Kifungo Mrisho alisema kuwa kabla ya kuwepo kwa machapisho hayo kumekuwepo na mchakato mrefu, ikiwemo kuingia katika Mahakama Mtandao na masuala ya TEHAMA ili kuwezesha kupata uamuzi wa mashauri mengi ya Mahakama Kuu Tanzania Bara na Visiwani sambamba na Mahakama ya Rufani, hatua ambayo imewezesha upatikanaji wa taarifa zote kuanzia mwaka 2007 mpaka 2020.

Uzinduzi wa Juzuu hizo umefanyika tarehe 24 Januari, 2022 katika Viwanja vya Nyerere Square vilivyopo katikati ya Jijini la Dodoma na kuhudhuriwa na watumishi pamoja na Viongozi mbalimbali wa Serikali wakiongozwa na Jaji Mkuu wa Tanzania Prof. Ibrahim Hamis Juma.




***Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Geofrey Mizengo akipokea maelezo ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na OWMS kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi Usimamizi wa Mashauri Bw. Abubakar.***

# Tuishi Katika Falsafa ya Kuboresha Utendaji Katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali



**Paul Nanai Kuyi**
**Afisa Ununuzi**

**Katika kuboresha utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa ikiandaa mafunzo ambayo yamesaidia kukutanisha watumishi wote kwa ajili ya kuongeza, kuboresha na kuimarisha utendaji ndani ya ofisi ya Wakili Mkuu.**

Miongoni mwa mafunzo yaliyowahi kuandaliwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni pamoja na mafunzo kuhusu kutambua na kubainisha viashiria hatarishi (risk management) na upimaji wa utendaji kazi kwa watumishi wa Umma (OPRAS) ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia kuongeza ufanisi katika utendaji wa kila siku hatua iliyopelekea kutimiza masharti na taratibu za kitendaji wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (compliance).

Kwa kutambua umuhimu wa mafunzo haya ofisi kupitia Idara ya Utawala na Rasilimali Watu iliandaa mafunzo ya utendaji na uendeshaji wa shughili za Ofisi ya Wakili Mkuuu wa Serikali mafunzo yaliyofanyika katika Ukumbi wa mikutano wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) uliopo Kibaha Mkoani Pwani. Mimi ni mmoja wa waliohudhuria mafunzo hay ana niliona kuna umuhimu wa kuwashirikisha wengine kwa kuandika Makala hii.

Kupitia hotuba Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt Boniphace Luhende aliyoitoa wakati akifungua mafunzo Dk. Luhende alisisitiza pamoja na mambo mengine, juu ya umuhimu wa kuendelea kutekeleza majukumu kwa kufuata Sheria taratibu na kanuni za utumishi wa umma katika kuhakikisha changamoto za masuala mbalimbali zinazoihusu ofisi yetu zinapatiwa ufumbuzi.

Pamoja na mambo mengine, Mh. Dk. Luhende aligusia mambo muhimu matano (5) ambayo tunapaswa kuyaishi kama watumishi kwa ajili ya kuleta mabadiliko na kuboresha utendaji wetu wa kazi huku akiwasihi watumishi waliohudhuria mafunzo hayo kuwa mambo haya tuyafanye kuwa falsafa ya utendaji wetu una kuyaainisha kama ifuatavyo.

Mosi, ni kuwa na mipango, Watumishi wengi hawana mipango. Bila ya kuwa na mipango inakosa uelekeo na mwisho tunapotea. Alisema inawapasa watumishi kuwa na mipango ambayo kama ofisi itasaidia kutekeleza mikakati kwa ufanisi pamoja na kutimiza malengo ya Serikali na taasisi kwa ujumla wake.

Ni vyema kila mwaka wa fedha unapoanza kila Idara na vitengo kuainisha mipango yao ambayo itatekelezwa kwa mwaka husika hatua hii itawezesha kupunguza malalamiko ambayo yamekuwa yakitolewa kwa wenzetu pale wanaposhindwa kupanga mambo yao vizuri nahivyo kuongeza ufanishi na kuwezesha Ofisi yetu kutimiza masharti na miongozo mbalimbali ya Serikali.

Pili ni kuwa na utaratibu; hatua hii itaisaidia ofisi yetu na Serikali kwa ujumla kufanya kazi kwa kuzingatia miongozo, Sheria, Kanuni na taratibu hivyo kwa kutumia mifumo tuliyonayo, wanapaswa kufanya kazi kwa kufuata kanuni na taratibu za utumishi wa umma hatua itakayosaidia kutekeleza majukumu yetu kwa weledi ikiwa ni pamoja na kutunza siri za ofisi yetu.

“Naomba watumishi wote tutumie mifumo hii katika kuendesha shughuli zetu za kila siku hii itatusaidia kufanya kazi kwa kufuata taratibu za utumishi Pamoja na kutunza siri za ofisi”. Alisema Dkt. Luhende.

Aidha aliwakumbusha watumishi wote umuhimu wa kusimamia na kutumia vizuri taratibu za kazi. Mathalani kwa kujiepusha na masuala ambayo yamekuwa yakifika juu pasipo kupitia kwa Wakuu wa Idara na Vitengo husika kwa kuwa utumishi wa Serikali unataka mambo yote yafuate utaratibu yaani ngazi kwa ngazi hivyo ni lazima Afisa Masuuli ayaone kwanza ndio ayarudishe chini kwa mtu anayehusika kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Pamoja na hilo Ofisi yetu kwa kiasi kikubwa imeboresha na inaendelea kuboresha mifumo ya kielektroniki, kama njia ya mfumo kuwasiliana kwa

kwenye majalada (e-Office). Naomba tujifunze namna bora ya kutumia mifumo hii kwa ajili ya kuharakisha maamuzi, Haya ndio mabadiliko katika Tehama ambayo tukiyatumia vizuri yatatusaidia kuboresha utendaji kazi wetu.

Tatu, Mawasiliano; suala hili ni muhimu sana, iwe mawasiliano ya ndani ya Ofisi ama nje ya Ofisi mawasiliano yoyote yana taratibu zake za kufuata, Kila tunapotekeleza majukumu yetu naomba tufanye mawasiliano kati yetu ili kupunguza vihatarishi (risks) ambavyo vitaleka madhara ama kuzua taharuki katika Ofisi. Mara kwa mara mawasiliano (Communicate and Consult), usijifanyie tu maamuzi peke yako wakati hii ni Taasisi Kwa sababu Jambo linapofanyika ndivyo sivyo inaonekana Ofisi haina ushirikiano.

Nne, Uwajibikaji, suala hili ni lazima ujue majukumu na mgawanyo wa kazi zako (Roles and position). Usipojua nafasi yako ni vigumu kutimiza wajibu wako. Katika eneo hili tuzingatie kutimza majukumu yetu kwa ufanisi na uharaka zaidi. Sifurahishwi kuona watumishi wanakaa na majukumu (tasks) muda mrefu pasipokuwa na sababu za msingi. Tujifunze kanuni inayosema kile cha kwanza (First Things First -Clear your desk). Lakini pia tuweze kujua jambo lipi ni la haraka na lipi la kusuburi. La haraka liende na la kusubiri lisubiri lakini kila wakati wasiliana (Communicate and Consult) ili tuweze kujua tumefikia hatua ipi.

Tano, maelekezo na udhabiti (direction and control). Kila tutakachokifanya Tukifanye kwa kufuata maelekezo mahsusi. Aidha baada ya kuwa umetekeleza jambo, jitahidi kufatilia kuona limefikia hatua ipi, kwa ajili ya kutoa mrejesho. Usifanye tu ilimradi ukajisemea nimelifanya limekwisha. Ni lazima tujue hatima ya mambo yanatupitia katika sehemu zetu (monitoring and control). Bila hivyo hatutaweza kujipima ni wapi umekosea kwa ajili ya kusahihisha na kuboresha kwa ufanisi katika kuendesha Ofisi yetu.

Tukitaka kufanikwa katika haya yote ni lazima tuzingatie kuwa na mipango Madhubuti katika maeneo yetu, kuwa wa moja (team-work/synergy), tutambue nafasi zetu, kuziheshimu na kuzitendea haki. Pia ni suala la muhimu kupata suluhisho (solution oriented) tunapotekeleza majukumu ili itusaidie kuepuka kufanya suala kuwa gumu ama kulalamika kila mara, toa suluhisho ama wasilana upate msaada. Suala la ubunifu (creativity) pia hatutaliacha nyuma lazima tuzingatie katika utendaji hivyo ni muhimu kuwa wavumilivu na kuvipa muda vitu ili vitokee kwa wakati kwa lengo la kupata matokeo chanya katika kila tunachokifanya.

***"Naomba watumishi wote tutumie mifumo (Mipango, Utaratibu, Mawasiliano, Uwajibikaji na Maelekezo na Udhabiti) katika kuendesha shughuli zetu za kila siku hii itatusaidia kufanya kazi kwa kufuata taratibu za utumishi Pamoja na kutunza siri za ofisi". Dkt. Boniphace N. Luhende***

# "Tuendelee Kufanya Kazi kwa Bidii" - Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wametakiwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii na moyo wa kujitolea huku wakifuata Sheria, Taratibu na Kanuni za Utumishi wa Umma ili kuiwezesha OWMS kufikia malengo waliyojiwekea.

Wito huo umetolewa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende wakati akizungumza na Watumishi wa OWMS katika hafla ya kutathimini utendaji kazi wa ofisi kwa mwaka 2021 na malengo ya ofisi kwa mwaka 2022.

Alisema kuwa mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka 2021 yamechangiwa kwa sehemu kubwa na ari waliyokuwa nayo watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kutekeleza majukumu yao kwa weledi. Dkt. Luhende amewashukuru watumishi kwa kushiriki kufanikisha mafanikio yaliyopatikana katika ofisi.

Alisema Ofisi imepokea fedha zinazotosha kununua magari 13, ununuzi wa kompyuta 126. Fedha hizo pia zitawezesha watumishi 59 kupandishwa madaraja, kuongezeka kwa idadi ya watumishi 51 na kufanya jumla ya watumishi kuwa 173 na kuwezesha, ukarabati wa jengo la OWMS pamoja ufunguzi wa ofisi za mikoani ikiwemo Mkoa wa Morogoro. Aidha aliwapongeza Watumishi wa OWMS kwa kupata hati safi ya Hesabu za OWMS kwa mwaka 2020/2021.



**Dkt. Boniphace N. Luhende**
**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

"Upande wa kuendesha mashauri tumefanikiwa kuhitimisha kwa njia ya majadiliano mashauri baina ya TAMISEMI na Kampuni ya Mawasiliano ya Vodacom na hivyo kufanikisha Serikali kulipwa kiasi cha Bilioni 6 na milioni 600 ambazo zilikuwa ni fedha taslimu zilizolipwa mwaka huu" alisema Dkt. Luhende.

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ameendelea kuwakumbusha watumishi kuwa na nidhamu na kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kuchukua hatua stahiki kwa mtumishi ambaye hatazingatia wajibu wake.

Dkt. Luhende ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuiamini ofisi na kuridhia kuongeza bajeti kutoka bilioni 11.4 kwa mwaka wa fedha 2020/21 mpaka bilioni 12.1 kwa mwaka wa fedha 2021/22 na kusema kuwa tunategemea kupata ongezeko la bajeti kwa mwaka ujao wa fedha hatua itakayosaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi.

Dkt. Luhende alisema kuwa hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa na ofisi kwa lengo la kuboresha maslahi ya watumishi hivyo amewataka watumishi kuwa wavumilivu katika kipindi chote ambacho mchakato huo unashughulikiwa kwa kuwa mambo mazuri yanakuja.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha ofisi hii inawaendeleza watumishi wake kielimu tayari ofisi imetoa ufadhili wa muda mrefu kwa watumishi wapatao 12 kwa maana ya Shahada ya kwanza na Shahada ya Uzamili na katika hili Ofisi ilihakikisha kila Idara inatoa mtu mmoja kwenda kwa ajili ya mafunzo haya.

"Kwa upande wetu sisi kama Ofisi tumejipanga vizuri tutahakikisha kila mtu anayesitahili kupata mafunzo haya anaenda shule labda mshindwe wenyewe". Alisema Dkt. Luhende.

Dkt. Luhende alisema kuwa vipaumbele vya mwaka ujao ni kuendelea kuboresha maslahi ya watumishi ikiwemo mishahara, nyumba, Mawasiliano, fedha ya Vazi la Mahakama pamoja na vitu vingine ambavyo vikiboreshwa vitasaidia kuongeza ari ya ufanyaji kazi.

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali alisema kuwa ofisi inaendelea na maandalizi ya ujenzi Jengo la Ofisi Makao Makuu Dodoma tayari tumepata ramani pamoja na BOQ na ujenzi huo unatarajiwa kuanza mapema.

Dkt. Luhende ameongeza kuwa ofisi inatarajia kufanya mkutano mkubwa wa watumishi wote kwa lengo la kujadili mipango mbalimbali ya ofisi ikiwa ni pamoja na kuendesha mafunzo mbalimbali ya Mawakili pamoja na Idara nyingine zilizoko katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Akihitimisha hotuba yake, Dkt. Luhende amewataka watumishi kuendelea kufanya kazi kama bidii kama timu moja pamoja na kumheshimu kila mmoja na kufanya kazi kwa weledi, upendo, furaha, amani, maridhiano, mshikano na hakika kwa kufanya hivyo juhudi hizo zitazaa matunda na matokeo yake tutayaona.



***Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakikata keki kuashiria kuaga mwaka 2021 katika viwanja vya ofisi jijini Dar Es Salaam***



***Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende akisalimiana na Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu katika halfa ya kufunga mwaka 2021 katika viwanja vya ofisi jijini Dar Es Salaam***



***Muonekano wa Mbele (front view) wa Jengo jipya la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali linalotarajiwa kujengwa katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma***



***Muonekano kwa upande (side view) wa Jengo jipya la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali linalotarajiwa kujengwa katika Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma***




***Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Prof Ibrahim Hamis Juma (katikati) akipitia vitabu vya mkusanyiko wa mashauri ya mahakama ya kazi***

# Jaji Mkuu Azindua Vitabu vya Mkusanyiko wa Maamuzi ya Mahakama ya Kazi

Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma amezindua Vitabu vya Mkusanyiko wa Maamuzi ya Mahakama ya Kazi (Labour Court Case Digest) na kuhimiza kasi ya usikilizaji wa mashauri na utatuzi wa migogoro ya kazi inayoletwa mahakamani ili kusaidia kuchochea ukuaji wa uchumi hapa nchini.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa Vitabu hivyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam, Jaji Mkuu alisema kuwa hakuna ubishi kwamba maendeleo ya mtu mmoja mmoja na kukua kwa uchumi wa nchi kwa ujumla kunategemea upatikanaji wa haki kwa wakati ambayo huchagizwa na umalizaji haraka wa migogoro inayowasilishwa Mahakamani.

Prof. Juma alibainisha kuwa sekta ya kazi ni moja ya sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi, hivyo kwa upekee, umalizaji wa haraka wa mashauri ya kazi yaliyopo katika ngazi mbali mbali za vyombo vya utatuzi wa migogoro ya kazi na utoaji haki ni moja ya nguzo muhimu katika ukuaji wa uchumi.

"Tulifanya Ugatuzi wa kuwapa mamlaka Majaji waliopo katika Kanda za Mahakama Kuu ndio maana mnamo mwaka 2018, hatua hii iliwawezesha kusikiliza mashauri ya kazi. Hii imesaidia umalizikaji haraka wa mashauri ya kazi sehemu zote ambazo kuna Kanda ya Mahakama Kuu," Jaji Mkuu alisema.

Aliongeza kuwa ili migogoro ya kazi iweze kutatuliwa kwa haraka na kwa wakati, ni sharti Mahakama itoe tafsiri ya sheria za kazi kupitia maamuzi mbalimbali ili kuwawezesha watatuzi wa migogoro kufanya maamuzi ya haki na kwa wakati.

"Vitabu hivi vitawezesha Mahakama na vyombo vingine vya kutoa haki katika sekta ya kazi pamoja na wadau wake kuleta urahisi wa rejea wakati wa usikilizaji na utoaji maamuzi wa mashauri ya kazi, pia vitabu hivi vitasaidia Waajiri na Wafanyakazi kujua zaidi mambo muhimu yaliyomo kwenye sheria za kazi kwa kuwa sheria hizo zimetafsiriwa katika vitabu hivi," alisema.

Jaji Mkuu alisema kuwa Mkusanyiko wa vitabu hivyo utatusaidia kupunguza migogoro katika sehemu za kazi na kuchochea kuongeza ufanisi katika utendaji kazi kwa kila mmoja kujua haki na wajibu alionao utakaopelekea kukua kwa uchumi nchini kwetu.

"Kwetu sisi Mahakama ni chombo cha Usuluhishi na Uamuzi, hivyo kupitia vitabu hivi tutakuwa na nafasi nzuri ya kuongeza kasi ya usikilizaji wa mashauri na hivyo itawezesha wananchi kupunguza muda katika kudai haki na badala yake kutumia muda mwingi katika uzalishaji mali," alisema Jaji Mkuu.

Kwa upande wake, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, Mhe. Salma Maghimbi alisema kuwa kwa mujibu wa kanuni ya 3(1)(a) ya Kanuni za Mahakama ya Kazi, Mahakama ina jukumu la kuweka kumbukumbu za




***Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma akimkabidhi vitabu vya mkusanyiko wa mashauri ya Mahakama ya Kazi Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt Boniphace Nalija Luhende***

maamuzi inayokuwa imeyatoa katika kutekeleza mamlaka yake, hivyo utekelezaji wa jukumu hilo ndilo chimbuko la kuwa na vitabu hivyo vya ripoti ya maamuzi ya Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi.

Mhe. Maghimbi alisema kuwa "Labour Court Case Digest" ni vitabu vinavyokusanya maamuzi mbalimbali yanayohusiana na ajira na mahusiano kazini, yaliyoamuliwa na Majaji wa Divisheni ya kazi na mashauri hayo hukusanywa kwa umahiri ili kujumuisha maamuzi yanayogusa masuala tofauti na yenye kutoa tafsiri na misimamo ya Sheria za kazi, Kanuni zilizopo pamoja na Mikataba ya Kimataifa inayohusiana na masuala ya kazi.

"Ukusanyaji huu hufanywa na watalaamu waliobobea katika Sheria na uwezo wa kufanya uchambuzi wa mashauri, kuyakusanya na kuyaripoti kwa namna ambayo itamnufaisha mlengwa," alisema Mhe. Maghimbi

Aidha, alibainisha kuwa dhumuni la uzinduzi wa vitabu hivyo ni kuongeza wigo wa ufahamu kwa wadau wote wa sekta ya kazi pamoja na jamii kwa ujumla, juu ya uwepo wa vitabu hivyo ambayo ni miongozo ya sheria katika kushughulikia na kutatua masuala mbalimbali katika sekta ya kazi ikiwemo migogoro inayotokana na mahusiano kazini.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Nalija Luhende akizungumza katika hafla hiyo ameipongeza Mahakama ya Tanzania, Divisheni ya Kazi kwa kazi nzuri inayofanya ya kutatua migogoro mbambali ya wananchi huku akimshukuru Mhe. Jaji Mkuu kwa kuialika OWMS kama mdau muhimu wa Mahakama kuhudhuria uzinduzi huu muhimu katika Sekta ya sheria nchini Tanzania.

Alisema kuwa Mahakama ya Tanzania hususani katika matumizi ya TEHAMA mfano mzuri kwetu sisi ni matumizi ya mfumo wa TanzLII ambako maamuzi mbalimbali ya Mahakama yamekuwa yakiwekwa huko kwa wakati na kwa kufanya hivyo imetuwezesha sisi wadau wa Mahakama kupitia mfumo huo kujipatia kwa urahisi maamuzi ya Mahakama zote nchini pamoja na nyaraka za sheria.

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali alisema kuwa ni wazi kuwa Serikali ndio muajiri mkubwa nchini hivyo jambo hili ndilo linalopelekea kuzalishwa kwa mashaurii ya kazi yanayotokana na hatua mbalimbali za kiutawala zinazochukuliwa na Serikali kama mwajiri, hatua hii inaifanya OWMS kama msimamizi wa Mashauri yote yanayofunguliwa dhidi ya Serikali kuwa mdau mkubwa sana wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi.

"Uzinduzi wa Mkusanyiko wa mashauri ya kazi ni hatua muhimu sana kwetu sisi kama wadau wa Mahakama, tunatambua wazi kwamba mkusanyiko huu utasaidia kupunguza mashauri ambayo hayana tija pale ambapo kuna maamuzi ya Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani kuhusu mienendo ya mashauri ya kazi". Alisema Dkt. Luhende.

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende ametoa wito kuwa, pamoja na kuleta uelewa kwa wadau na taratibu mbalimbali za kimahakama tunatarajia kuwa mkusanyiko wa maamuzi haya pia utaweza kupatikana kwa urahisi na ikiwezekana kwenye nakala laini (soft copy) ili kuwezesha wadau kuipata kwa urahisi Zaidi.

Dkt. Luhende alimuomba mgeni rasmi Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma kuwa pamoja na kwamba OWMS inatambua jitihada za wazi zinazofanywa na Mahakama ya Rufani katika kumaliza Mashauri kwa wakati aliomba kuwe na kikao

maalum kuhusu Mashauri ya kazi (Special Session) ili kusaidia kupata maamuzi ya Mahakama ya Rufani ambayo yanatoa msimamo wa tafsiri ya sheria ambazo zinamaamuzi kinzani.

"Kama jambo hili litakupendeza Mhe. Mgeni Rasmi basi OWMS na wadau wengine tuko tayari kushirikiana na Mahakama kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa ili kuweza kupata suluhu na ufafanuzi muhimu wa Mahakama ya Rufani katika maamuzi yote kinzani" alisema Dkt. Luhende

Dkt.Luhende alimshukuru Mhe. Jaji Mkuu huku akiahidi kuwa OWMS itaendelea kudumisha uhusiano uliopo kati yake na Mahakama ili kusaidia upatikanaji wa haki kwa Serikali na kwa watanzania wote kwa ujumla.

Hafla ya uzinduzi wa Mkusanyiko wa Vitabu vya Maamuzi ya Kazi, imehudhuriwa na maafisa mbalimbali wa Mahakama ya Tanzania, akiwemo Kaimu Jaji Kiongozi, Mhe. John Mgetta na Jaji Mfawidhi wa Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki Temeke, maalumu kwa mashauri yanayohusu ndoa na talaka, Mhe. Ilvin Mugeta.

Wageni wengine waliohudhuria hafla hiyo ni Mkuu wa Shule ya Sheria, ambaye pia ni Jaji wa Mahakama Kuu, Mhe. Dkt. Benhajj Masoud, Mkurugenzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Kazi (ILO-Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi), Bw. Wellington Chibebe, Majaji mbalimbali wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mawakili wa Serikali na wadau mbalimbali wa Mahakama ya Tanzania.



***Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma (katikati walioketi) akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi waliohudhuria halfa ya uzinduzi wa vitabu vya mkusanyiko wa Maamuzi ya Mahakama ya Kazi***



**Mhe. George Simbachawene**
**Waziri wa Katiba na Sheria**

# Waziri Simbachawene Akutana na Viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali Gabriel Malata, wamemtembelea na kufanya mazungumzo na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. George B. Simbachawene kwa lengo la kujitambulisha na kumueleza jinsi ofisi hiyo inavyotekeleza majukumu yake.

Akizungumza wakati wa kikao hicho Mhe. Simbachawene amewashukuru Viongozi kwa kufika ofisini kwake huku akiwasihi kuendelea kuchapa kazi kwa bidii ili wote kwa pamoja waweze kufikia malengo waliyojiwekea.

Mhe. Simbachawene ameongeza kuwa ni muhimu kwa kila Taasisi iliyoko chini ya Wizara yake kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwani kwa kufanya hivyo kutaisaidia Serikali kuharakisha maendeleo kwa wananchi wake kupitia sekta ya sheria.

Alisema kuwa katika kipindi kifupi tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ofisi hii imesaidia Serikali kuokoa fedha nyingi kwa kuwa ufanisi umeongezeka katika uendeshaji wa mashauri ya Serikali hatua iliyopelekea kiasi kikubwa cha fedha kuokolewa na kuelekezwa katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

“Kila Taasisi ni vyema ikatekeleza majukumu yake kwa mujibu ya sheria, taratibu na kanuni ili tuweze kuisaidia Serikali kuwaletea

maendeleo wananchi kupitia sekta ya Sheria." Alisema Simbachawene.

Aidha Mhe. Waziri ameahidi kuzichukua na kuzifanyia kazi changamoto zote zilizowasilishwa na Viongozi hao hatua itakayosaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku mara tu zitakapotatuliwa.

Wakieleza changamoto zinazowakabili wamezitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni ufinyu wa bajeti, ukosefu wa vitendea kazi kama vile umiliki wa majengo ya ofisi, Magari ya kutosha, pamoja na upungufu wa watumishi.

Naye Naibu Waziri Wizara ya Katiba na Sheria Mhe. Geofrey Mizengo Pinda, ameipongeza OWMS kwa kufanya kazi kwa bidii na kuahidi kuendelea kuwa kiungo muhimu kati ya Taasisi hizo na Wazara ili kuhakikisha Taasisi hizo zinatimiza malengo yao waliyojiwekea kulingana na mpango kazi wa Taasisi zao.

Kwa upande wao viongozi hao wakiongea mara baada ya kumalizika kwa Kikao kazi hicho wamemshukuru Mhe. Waziri kwa kukubali kukutana nao ili waweze kuzungumzamambo mbalimbali ambapo viongozi hao wametumia fursa hiyo kumuuleza majukumu ya ofisi na namna wanavyoyatekeleza.

Kikao hicho kimefanyika katika ukumbi wa mikutano wa Wizara ya Katiba na Sheria uliopo Mtumba Jijini Dodoma, kimewahusisha Viongozi wa Tasisi kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.



***Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. George Simbachawene (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walipofika kujitambulisha ofisini kwake jijijni Dodoma***

# Ofisi ya Wakili Mkuu ya Serikali Yapongezwa Tanga



**Bi. Spora Liana**
**Mkurugenzi wa Jiji la Tanga**

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mkoani Tanga imepongezwa kwa usimamizi mzuri wa Mashauri ya Serikali na Taasisi zake kwa kuweza kusaidia kuwajengea uwezo Mawakili wa Taasisi nyingine katika kuandaa na kusimamia Mashauri dhidi ya Taasisi zao.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga Bi Spora Liana ofisini kwake wakati akihojiwa na waandishi wa Jarida hili waliotaka kujua ofisi yake imenufaika vipi na uwepo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mkoani humu.

"Toka ulipoanza utaratibu huu wa kushirikiana kati ya Taasisi za Serikali na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali tumeona kuna tija kubwa na manufaa mengi katika usimamizi wa mashauri ya Serikali na mabadiliko makubwa kwa wanasheria wetu wa taasisi". Alisema Liana

Liana alisema kuwa asilimia kubwa ya mashauri ambayo yanafunguliwa sasa dhidi yao Serikali inashinda na kuepuka gharama za kulipa fidia na fedha hiyo kwenda kutumika kwenye miradi ya maendeleo kwenye taasisi wanazofanyia kazi.

***"Toka ulipoanza utaratibu huu wa kushirikiana kati ya Taasisi za Serikali na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali tumeona kuna tija kubwa na manufaa mengi katika usimamizi wa mashauri ya Serikali na mabadiliko makubwa kwa wanasheria wetu wa taasisi".***

Alieleza kuwa wamekuwa wakifanya vikao vya usuluhishi mara kwa mara kati ya Halmashauri, Ofisi ya Wakili Mkuu na watu wanaofungua mashauri ya madai dhidi ya halmashauri kujadiliana na kukubaliana namna ya kupunguza gharama ambazo zinatakiwa zilipwe kwa wahusika.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Sheria Wakili Sebastian Danda alisema Halmashauri ya Jiji la Tanga wamekuwa ndio wanufaika wakubwa tangu takwimu za miaka miwili iliyopita tumepokea mashauri manne (4) tu dhidi ya Serikali na mpaka sasa hatuna mashauri mengine mapya ambayo yamefunguliwa dhidi yetu" alisema Danda.

Danda alisema kuwa kuna mafanikio mengi ambayo yametokana na uwepo wa ofisi hii kwenye Halmashauri ya Jiji ikiwemo kupunguza gharama za kutumia Mawakili binafsi kwenye mashauri ya mahakamani na kupunguza kuwakilishwa kwa halmashauri kama tungeshindwa kwenye kesi za madai zilizofunguliwa dhidi yetu". Alisema Danda.

Ameongeza kuwa walikuwa na kesi za madai makubwa ya fidia za ardhi kama Shauri la Mohamedi Isa Mtalamile na wenzake wanne (4) shauri la uwakilishi wa wananchi 190 wakazi wa eneo la Pande dhidi ya Halmashauri ya Jiji la Tanga na Kiwanda cha Saruji Tanga ambapo walikuwa wanadai fidia ya ardhi Kiasi cha shilingi billion 7.3.

Aidha, Danda aliitaja kesi

**Bw. Rashid Said**

**Wakili wa Serikali Mfawidhi Tanga**




kuanzishwa kwa ofisi hii mkoani humo kwa kuweza kupunguza idadi ya mashauri yanayofunguliwa dhidi ya ofisi tofauti na kipindi ambacho hakukuwa na Ofisi ya Wakili Mkuu.

"Idadi ya mashauri ambayo yanafunguliwa dhidi ya halmashauri inazidi kupungua mwaka hadi mwaka na kwa mahakamani pindi wanasheria wanapata dharura.

"Sisi kama Halmashauri ya Jiji tumekuwa wanufaika wa kubwa tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Tanga kwa kufanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 11.5 ambazo tulitakiwa kuzilipa kwa wananchi kama fidia za ardhi nyingine ya Bakari Mbuguni na Wenzake 222 wakazi wa eneo la Magaoni dhidi ya Halmashauri na Self Investment ambapo walikuwa wanadai fidia ya kiasi cha shilingi bilioni 4.2 baada ya kuondolewa kwenye eneo walilokuwa wamevamia na kuvunjwa kwa nyumba zilizokuwa zimejengwa kwenye eneo hilo mwaka 2006.

Naye Wakili wa Serikali Mfawidhi Mkoa wa Tanga Bwana Rashid Mohamed Said alisema kuwa takribani taasisi zote za Serikali mkoani Tanga zimekuwa zikiitumia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kama msuluhishi na kuweza kupata mafanikio makubwa hasa halmashauri na taasisi za mifuko ya hifadhi za jamii.

Said alisema kuwa kwa muda mfupi toka kuanzishwa kwa ofisi hii mkoani Tanga wamekuwa wakipata ushirikiano mzuri kutoka kwenye taasisi zote za Mkoa huo jambo ambalo limerahisisha kuongeza tija katika kusimamia mashauri dhidi ya Serikali na kusaidia kupunguza gharama kubwa za kutumia mwakili binafsi.

"Changamoto tunayoipata ni baadhi ya taasisi kuchelewa kutoa taarifa muhimu za undeshaji wa mashauri yaliyopo mahakamani na kutupa wakati mgumu wa kusimamia Serikali husika, tumeshanza kukaa na taasisi hizo kwa ajili ya kuwaeleza umuhimu wa kutoa taarifa za mashauri mapema" alisema Said.

Ameongeza kuwa moja ya jukumu kubwa la ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mkoa wa Tanga ni kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi yanayoihusu Serikali ambapo kumekuwa na mashauri 105 ambayo yalifunguliwa toka kuanzishwa kwa ofisi hii mwaka 2018 na tayari mashauri 76 yamemalizika katika nyakati tofauti na bado tunaendelea na mashauri 26 katika mahakama mbalimbali.

Alieleza kuwa mafanikio hayo yametokana na ushirikiano mzuri uliopo kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu kwa kutoa ushauri kabla ya mashauri hayajafunguliwa na kusimamia mashauri ambayo yapo mahakamani dhidi ya taasisi husika.

Said alieleza kuwa mafanikio waliyoyapata ni kuweza kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 13.8 kwa kufanikiwa kuiwakilisha vyema Serikali mahakamani na kushinda mashauri mbalimbali yaliyofunguliwa dhidi yake.

"Kiasi hiki cha fedha ni kile kilichookolewa ambacho Serikali ingeshindwa ilitakiwa illipe fidia kwenye mashauri mbalimbali yaliyofunguliwa dhidi yake na kwa hapa Tanga mengi yalikuwa ni mashauri ya fidia juu ya ardhi na madai ya watumishi waliondolewa kwenye utumishi wa umma kwa sababu mbalimbali". Alisema Said.

Alieleza kuwa mafanikio hayo yametokana na ushirikiano mzuri uliopo kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu kwa kutoa ushauri kabla ya mashauri hayajafunguliwa na kusimamia mashauri ambayo yapo mahakamani dhidi ya taasisi husika.

Alisema kuwa Kwa kipindi cha miaka minne Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuongeza ufanisi kwa kuboresha ushirikiano katika taasisi za Serikali na kufanikiwa kuokoa kiasi hicho cha fedha ambacho kama sio kwa ushirikiano Serikali ingeshindwa mashauri na kupoteza kiwango hicho cha fedha.



**Sebastian Danda**

**Mkuu wa Kitengo cha Sheria Halmashauri ya Jiji Tanga**

# Shauri Dhidi ya Wakala wa Majengo Latupwa

**Wakili wa Serikali Bw. Camillius Ruhinda**



Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) imetupilia mbali shauri la mgogoro wa kikazi lililofunguliwa na Bw. Joseph Chedego na wenzake 48 dhidi ya Wakala wa Majengo (TBA) wakidai zaidi ya shilingi milioni 500 kama stahiki zao za ajira zisizo halali za ujenzi wa majengo ya Serikali.

Uamuzi huo umetolewa na Msuluhishi Neema Njiwa kutoka Tume ya Usuluhishi baada ya Chedego na wenzake kupeleka maombi yao nje ya muda wa Tume. Hii ni kufuatia Wajibu Maombi kuweka pingamizi la kutomjumuisha Mwanasheria wa Mkuu wa Serikali katika mgogoro huo.

Msuluhishi Njiwa alisema kuwa waleta maombi hawakuwa sahihi kudai pingamizi lililowasilishwa awali dhidi yao ndio lilipelekea kuchelewesha mgogoro huu. Alisema Waleta Maombi wameshindwa kutoa sababu ya msingi iliyowapelekea wakashindwa kufungua upya shauri lao ndani ya siku 14 kama walivyoagizwa.

“Natupilia mbali maombi haya baada ya Tume kuona waleta maombi hawakuwa na sababu za msingi za kushindwa kufungua mgogoro wao ndani ya muda wa siku 14 walizopewa na Tume ikizingatia historia ya shauri hili toka lianze”. Alisema Njiwa.

Awali akielezea Tume kuhusu maombi hayo, Wakili wa Waleta Maombi Wakili Zakaria Kanyana alisema kuwa waleta maombi walikuwa ni wafanyakazi wa Wakala wa Majengo kuanzia tarehe 1/10/2017 na mgogoro ulitokea 15/01/2020 na uliwasilishwa kwenye tume ndani ya siku 30.

Wakili Kanyana alisema waleta maombi walifanya kazi masaa kumi na mbili (12) kwa siku bila likizo na kulipwa stahiki zao na wamechelewa siku ishirini nne ambazo hazitaweza kuathiri upande mwingine.

“Waleta maombi wapo ndani ya muda kwa kuwa ucheleweshaji ulisababishwa na sababu za kiufundi, naomba wapewe muda kwa kuwa mgogoro huo ni kwa ajili ya haki yao ya msingi hivyo waleta maombi sio wazembe kama inayooneka”, alisema Wakili Kanyama.

Aidha alisema Kiapo cha Waleta Maombi kipo vizuri na kudai kuwa taratibu za kiapo katika Mahakama nyingine zipo tofauti na za Tume, na waleta maombi wana matarajio makubwa kushinda mgogoro huu kwa kuwa waleta maombi walifanya kazi na TBA masaa ya ziada bila malipo yoyote na kuachishwa kazi bila sababu yeyote.

Wakili wa Serikali Bw. Camillius Ruhinda alieleza Tume kuwa Wakili wa Waleta Maombi hakutoa sababu za msingi za kueleza kwanini walipewa muda wa siku 14 na Tume ili waweze kuwasilisha maombi yao upya na kushindwa kuyawasilisha na kusema waleta maombi walikuwa ni wazembe.

Ruhinda alisema kuwa shauri hili limechukua muda mrefu kusikilizwa kwa kuwa upande wa waleta maombi walishindwa kuhudhuria vikao kadhaa kwa kutoa sababu ya kuuguliwa na wakili wao na kushindwa kuthibitisha ukweli wa suala hilo pasina shaka.

“Naiomba Tume kutupilia mbali Mgogoro huu kwa kuwa Upande wa wajibu Maombi unatumia muda mwingi na gharama kubwa kufuatilia mgogoro huu” alisema Wakili Ruhinda.

Akitoa uamuzi kuhusu shauri hilo, Msuluhishi hakukubaliana na hoja za Wakili wa waleta maombi na hivyo kuyatupilia mbali.




*Picha ya pamoja ya baadhi ya Wanawake wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani*

# Ofisi ya Wakili Mkuu Yashiriki Maadhimisho ya Kilele cha Siku ya Wanawake Duniani

Wanawake kutoka ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wameshiriki maadhimisho Siku ya Wanawake Duniani mwaka 2022 yaliyofanyika katika viwanja vya Uhuru Jijini Dar es Salaam.

Tarehe 8 Machi ya kila mwaka ni Siku ya Wanawake duniani. Siku hii inaadhimishwa kwa lengo la kukumbushia na kutafakari juu ya matokeo ya kisiasa, kijamii, kiuchumi waliyofikia wanawake na msimamo wao imara katika ngazi ya kijamii kwa ujumla.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameitumia siku ya wanawake duniani kuwapongeza wanawake kote nchini kwa jinsi wanavyojitoa katika kujenga uchumi wa Tanzania.

Pongezi hizo amezitoa Mjini Unguja katika viwanja vya Maisara wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya siku ya wanawake duniani na kuhudhuriwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

"Katika siku hii ya Wanawake Duniani, nawapongeza wanawake wote kwa mchango wenu katika kujenga uchumi, kustawisha jamii na kudumisha Amani na utulivu" alisema Mheshimiwa Rais. Kaulimbiu ya siku hii muhimu ni "Kizazi cha Haki na Usawa kwa Maendeleo Endelevu:Tujitokeze Kuhesabiwa". Haya yalisemwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwa ni siku chache kuelekea mwaka mmoja wa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano chini yake, ulionesha mafanikio makubwa kwa wanawake kupewa nafasi za uongozi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti Wanawake kutoka ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walisema mafanikio yoyote yanayoonekana hapa nchini na duniani kote kwa kiasi kikubwa yamechagizwa na uwepo wa wanawake.

Wanawake hao wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Rais mwanamke wa kwanza hapa nchini Tanzania na kwa kuendelea kuwaamini wanawake katika nafasi mbalimbali za kiuongozi kwenye Serikali yake.

Afisa Utumishi wa Ofisi wa Wakili Mkuu wa Serikali Neema Baltazary ameupongeza Uongozi wa ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kutambua na kuwapa nafasi Wanawake kufanya kazi katika Idara mbalimbali zilizopo ndani ya ofisi hali inayoonyesha kuzingatiwa kwa haki zao kwa kuwa mwanamke anao uwezo na ujasiri katika kuthubutu kufanya na kuleta mabadiliko hivyo kupewa kwake nafasi ni dhahiri kunachangia katika safari ya uboreshaji wa huduma za utoaji haki kwa wananchi.

"Napenda kutoa pongezi kwa Viongozi wa Ofisi hii kwa niaba ya Wanawake kwa kuweza kutoa nafasi mbalimbali za uongozi na kuendelea kuzingatia misingi ya haki za usawa na kuwaamini baadhi ya Mawakili wa Wanawake kusimamia mashauri makubwa yenye maslahi maslahi makubwa kwa taifa" Alisema Baltazary

Ameongeza kuwa imeonyesha dhahiri nafasi ya wanawake katika Ofisi ya Wakili Mkuu inaendelea kuchangia mafanikio ya ofisi na kuwataka wanawake kuendelea kutambua nafasi na uwezo walionao na kuzitumikia kwa ari na ujasiri kwa kuamini kuwa wana uwezo zaidi ya walio nao na kuleta mabadiliko kwenye nafasi hizo.

Katibu wa Chama cha Wanawake Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Bibi Jesca Kiggundu ametoa rai kwa watumishi Wanawake kusimamia nafasi zao kikamilifu na kuweza kusaidia katika kuboresha usimamizi wa mashauri yanayoihusu Serikali ili kutimiza malengo ya ofisi na Serikali kwa ujumla.

Kiggundu amewataka wanawake kuendelea kutafakari maendeleo ya jamii kwa kuzingatia misingi ya haki ili kutambua mchango wao wa maendeleo endelevu katika Nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa sababu tayari Serikali imeweka mifumo imara iliyoweza kubadilisha taswira na mitazamo hasi ya usawa wa kijinsia na masuala mapana ya haki ya mwanamke.

Ametoa wito kwa wanawake na watanzania kushiriki Sensa ya watu na makazi itakayofanyika mwaka huu ili kuiwezesha Serikali kupanga mipango sahihi ya maendeleo kwa wananchi katika maeneo yao.

Siku ya wanawake duniani ilianza kutokana na jitihada za wanawake 15,000 mwaka 1908 walipoandamana mjini New York Marekani wakidai kupunguziwa muda wa kufanya kazi, ujira wa kuridhisha na haki ya kupiga kura. Kilikuwa ni chama cha kisoshalisti cha Amerika kilichotangaza kuwa ni siku ya kwanza ya kitaifa ya wanawake, mwaka mmoja baadaye. Wazo la kuwa siku ya kimataifa lilianzishwa na mwanamke kwa jina la Clara Zetkin. Yeye alipendekeza wazo hilo mwaka 1910 katika mkutano wa kimataifa wa wafanyakazi wanawake huko Copenhagen Denmark.



# Toeni Majalada – Mkuu wa Wilaya Ilala




**Mhe. Ngw'ilabuzu Ludigija**
**Mkuu wa Wilaya ya Ilala**

> **"Haki ni stahiki ya kile kitu unachostahili kukipata na unapoifikisha mahakamani inachakatwa kupitia Ushahidi na mwisho wa siku inajulikana haki ni ya nani. Aidha, dhana ya haki ina pande mbili ambazo ni kushinda pale unapostahili na kushindwa pale ambapo haustahili na TEHEMA inatusaidia kufikia kwa uwazi na uharaka haki zote mbili."**

Serikali imetoa wito kwa Maafisa Upelelezi Mikoa na Wilaya kuhakikisha hawakai na majalada ya watuhumiwa kwa muda mrefu kwa ajili ya kuwawezesha Mawakili wa Serikali kufanyia kazi kwa haraka ili kupunguza mlundikano wa watuhumiwa mahabusu na pia kupunguza kazi zisizokuwa na mantiki kwa majaji.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala Ngw'ilabuzu Ludigija wakati wa Uzinduzi wa maadhimisho ya wiki ya Sheria Kanda ya Dar es Salaam yaliyofanyika katika viwanja vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu yakitanguliwa na maandamano kuanzia viwanja vya Mahakama Kuu hadi Kisutu.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Dalaam, Ludigija alisema magereza yana mahabusu wengi ambao wanaipa Serikali mzigo mkubwa.

"Serikali inatambua kuwa na mlundikano wa mashauri uliopo unaweza kukusababishwa na wadau waliopo kwenye mahakama kama jeshi la polisi, wandesha mashtaka au mawakili wa Serikali kwa kutambua hili ndio maana tunawataka hawa wadau wetu kufanya upelezi haraka ili kupunguza idadi ya mahabusu magerezani alisema.

"Niwaombe mhakikishe kuwa upelelezi unafanyika mapema kabla shauri halijapelekwa mahakamani na kuondoa mashauri yasiyokuwa na ushahidi kwa ajili ya kupunguza kazi zisizokuwa na mantiki kwa majaji na hatimae waweze kusikiliza kesi zenye ushahidi kwani magereza yetu wamejaa watu ambao wengine hawana sifa za kuwa gerezani". Alisema Ludigija.

Aidha, Ludigija alisema Serikali imefanya maboresho makubwa sana upande wa mahakama kuanzia majengo hadi kwenye kuendesha kesi kwa njia ya mtandao, ameipongeza mahakama kwa kuendesha mashauri mengi na mengine yakiwa yanaendelea kwa njia ya mtandao kwani imesaidia kupunguza mlundikano wa mashauri na kubaki na asilimia 15 za mashauri ambayo yamekaa kwa muda mrefu.

Alisema, kwa sasa malalamiko ya wananchi yamepungua kuhusu kucheleweshwa kwa kesi ama kuchelewa kutolewa maamuzi wa mashauri yao au kutotendewa haki ukilinganisha na kipindi cha nyuma lakini kwa sasa malalamiko hayo hawayaoni kwa upande wa pili isipokuwa yamebakia malalamiko kwenye mabaraza ya Ardhi.

Alisema, kuna changamoto



***Baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali waliohudhuria kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Sheria Kanda ya Dar es Salaam***

kubwa kwenye kesi zinazohusiana na ardhi hivyo anawaomba Wanasheria na mawakili waangalie Uwezekano wa kuboresha.

"Zipo changamoto nyingi sana kwenye kesi za ardhi hasa kwenye mabaraza, wasimamizi wa mabaraza haya waangalie namna gani wanaweza kuwasimamia hawa watu na kama kuna uwezekano basi wawekwe watu wengine ambao wako kisheria zaidi " alisema Ludigija.

Ludigija aliomba mahakama kuangalia kama kuna namna ya kuweka kwenye mlolongo mahakama za kawaida hizi kesi za Ardhi kwa kuwa zingesaidia kupunguza malalamiko. Aidha ameshauri kuwe na mabadiliko ikiwezekana kuwa na wanasheria waliosomea kabisa ili waweze kusaidia eneo hilo ambalo limekuwa na changamoto kubwa

Alisema, licha ya maboresho makubwa yaliyofanywa na Serikali pamoja na mahakama ya kuboresha miundombinu za majengo ya mahakama, bado kuna changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na baadhi ya mahakama kama vile Mahakama ya Temeke na ya Jiji kutumia majengo ya Serikali.

Kwa upande wake, Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Kanda Dar es Salaam, Amir Mruma alisema, katika wiki ya sheria ambayo inaashiria kuanza mwaka mpya wa mahakama, watatoa elimu kwa umma kuhusu sheria haki zake katika kiwango cha msingi kwa mwananchi atakayependa kujua haki zake.

Jaji Mruma alisema, haki ni stahiki ya kile kitu unachostahili kukipata na unapoifikisha mahakamani inachakatwa kupitia ushahidi na mwisho wa siku inajulikana haki ni ya nani. Aidha, dhana ya haki ina pande mbili ambazo ni kushinda pale unapostahili na kushindwa pale ambapo unastahili na TEHEMA inatusaidia kufikia kwa uwazi na uharaka haki zote mbili.

Alisema, Mwananchi anaposhindwa kesi ndani ya nafsi yake anajua ni haki yake kushindwa basi aridhike ndani ya moyo wake na kushindwa kwake kwa sababu haki itakuwa imetendeka anapaswa kuelewe kuwa dhana ya haki ni kushinda panapostahili na kushindwa unapostahili.

Vile vile aliwatahadharisha Waheshimiwa majaji na mahakimu, kutokana na maendeleo makubwa ya TEHAMA ambayo ndiyo mapinduzi ya Viwanda yanazungumziwa kwa mustakaba wa mahakama kuwa wanabidi wawe makini sana katika kupokea na kuchakata ushahidi wa kieletroniki maana inaweza kupotosha ukweli.

" Maendeleo hayo hayo ya teknolojia yana hasi yake na chanya yake kwa sababu watu wema watatumia teknolojia ikawa chanya na watu waovu watatumia teknolojia kwa uovu wao ikawa hasi, mfano kwenye mitandao ya kijamii kuwa kuna uwezekano wa kumuona mtu unayemfahamu lakini kwa uhalisia siyo yeye, tuwe makini kuitumia teknolojia kwa uchanya wake na Kuipuuza pale ambapo imetumika kwa hasi yake" Mruma

Aidha aliongeza kuwa, utoaji huduma kwa njia ya TEHAMA umesaidia katika upatikanaji haki , kuongeza uwezo kupunguza gharama mbali mbali na kuondoa vitendo vya rushwa.

"Katika Kanda ya Dar es Salaam zaidi ya mashauri 1871 kati ya 2225 yalisajiliwa kwa njia ya mtandao ambayo ni sawa na 84% huku kwa mwezi Desemba pekee mashauri 798 yalisikilizwa kwa video conference na kuifanya Kanda ya Dar es Salaam kuongoza kwa kusikiliza mashauri mengi kwa mwezi huo wa Desemba na kufikia 6352.



*Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Balozi Hussein Kattanga akisikiliza maelezo ya shughuli za OWMS kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi Usimamizi wa Mashauri Bw. Abubakar Mrisha kwenye viwanja vya Nyerere Square Dodoma*



*Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma akipokea maelezo ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na OWMS kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi Usimamizi wa Mashauri Bw. Abubakar Mrisha*

# Mahakama - Sio Kila Kesi ya Kikatiba Inaweza Kufikishwa Mahakamani



**George Nathaniel Mandepo**

**Mkurugenzi wa Usuluhishi**

Mnamo tarehe 15 Februari, 2022, Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Masijala Kuu, Kanda la Dar es Salaam ilitoa uamuzi katika Shauri la Kikatiba Na. 9 la mwaka 2021 baina ya Onesmo Olengurumwa dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Shauri hili lilifikishwa Mahakamani hapo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977(“Katiba”) kama ilivyorekebishwa mara kwa mara pamoja na Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Msingi Sura ya 3, Sheria ya Marejeo ya Sheria ya mwaka 2019 (“Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu”).

Katika Ombi hili ambalo lilisikilizwa na Mheshimiwa Jaji Elinaza Luvanda, Mhe.

Jaji Yose Mlyambina na Mhe. Jaji Stephen M. Magoiga, Mwombaji Wakili Onesmo Olengurumwa, alikuwa anapinga vifungu Na. 4(2); 4(3); 4(4), na 4 (5) vya Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu.

Mwombaji kupitia hati ya maombi alidai kwamba, vifungu hivyo vya Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu vipo kinyume na Katiba na ni batili na vinastahili kufutwa kwenye vitabu vya sheria za nchi. Mwombaji alieleza kuwa masharti yaliyomo kwenye Sheria husika yanapingana na Katiba na yanajaribu kwa kupitia mlango wa nyuma kurekebisha Katiba hasa Ibara ya 26 (2) na au kuweka katika Katiba matakwa ambayo hayakwekwa wala kuzingatiwa na Katiba.

Kupitia maombi hayo, Mwombaji aliitaka Mahakama itoe Amri kwamba: Moja, Vifungu vya 4(2), (3), (4); (5) vya Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu kama ilivyorekebishwa kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Na. 3 of mwaka 2020 haviendani na matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukiuka Ibara ya 13(2) na 13(4), 13(6)(a), 26(1) na 26(2) ya Katiba. Mbili, kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu kama iliyorekebishwa kina kinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukiuka Ibara ya 26(2) na 30(3) ya Katiba.

Tatu, Kifungu cha 4(4) cha Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu kama ilivyorekebishwa hakiendani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukiuka Ibara ya 26(1), 13 (2), na 13 (6) (a) ya Katiba. Nne, kifungu cha 4(5) cha Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu kama ilivyorekebishwa haiendani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukiuka Ibara ya 13(6)(a) na 26(1) ya Katiba.

Kwa upande wake, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uwakilishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali alipinga maombi hayo kwa kudai kuwa hayana msingi wa kisheria na yalistahili kufutwa mahakamani hapo. Kwa ufupi, kifungu cha 4 cha Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu kama ilivyorekebishwa mwaka 2020 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 kiliongeza vifungu vipya vya Sheria ambavyo ni kifungu cha 4(2),4(3),4(4) na 4(5).

Kwanza, Kifungu cha 4(2) kiliigizwa kwenye Sheria ili kuweka masharti ya kuzingatiwa kabla ya Mahakama Kuu ya Tanzania kukubali kesi ya kikatiba kifugu hiki kinaeleza kuwa, pasipo kuathiri masharti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, maombi chini ya kifungu kidogo cha 4(1) cha Sheria hiyo hayatapokelewa na Mahakama Kuu isipokuwa kama yawe yameambatana na hati ya kiapo inayoeleza ni kwa kiasi gani ukiukaji wa masharti ya Ibara ya 12 hadi 29 ya Katiba umemgusa Mleta maombi yeye binafsi.

Pili, Kifungu cha 4(3) kinatamka kuwa, mtu anayedai haki chini ya Ibara ya 26(2) ya Katiba atatakiwa kufuata masharti ya Ibara ya 30(3) ya Katiba. Tatu, kwa upande mwingine, kifungu cha 4(4) kinaeleza kuwa, pale ambapo shauri litafunguliwa dhidi ya Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Spika, Naibu Spika au Jaji Mkuu kwa kitendo au kasoro yoyote iliyofanywa katika utekelezaji wa majukumu yao, maombi yatapaswa kuwasilishwa tu dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mwisho, kifungu cha 4(5) kinaeleza kuwa, Mwombaji atalazimika, kabla ya kutafuta nafuu ya kisheria Mahakamani chini ya Sheria hiyo, atatakiwa kutafuta kwanza suluhu zote mbadala zinazopatikana chini ya sheria yoyote nyingine iliyotungwa na Bunge.

Ifahamike kuwa, Ibara ya 13(2) ya Katiba ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza kuwa, "Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake."Kwa upande mwingine, Ibara ya 13(4) inaeleza kuwa, "Ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa na mtu au mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi au shughuli yoyote ya Mamlaka ya Nchi."

Ibara ya 13(6) inasema"Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria, Mamlaka ya Nchi itaweka taratibu zinazofaa au zinazozingatia misingi kwamba (a) wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa mahakama au chombo kinginecho kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu, na pia haki ya kukata rufaa au kupata nafuu nyingine ya kisheria kutokana na maamuzi ya mahakama au chombo hicho kingenecho kinachohusika".

Ibada ya 26(1) na (2) za Katiba zinaeleza kuwa,"(1) Kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii Katiba hii na sheria za Jamhuri ya Muungano.(2) Kila mtu ana haki, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria, kuchukua hatua za kisheria kuhakikisha hifadhi ya Katiba na sheria za nchi".

Aidha, ibada ya 30(3) inaeleza kuwa"Mtu yeyote anayedai kuwa sharti lolote katika Sehemu hii ya Sura hii au katika sheria yoyote inayohusu haki yake au wajibu kwake,limevunjwa,linavunjwa au inaelekea litavunjwa na mtu yeyote popote katika Jamhuri ya Muungano,anaweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu."

Katika kujibu madai hayo, upande wa Serikali ulieleza kuwa Vifungu vinavyolalamikiwa vya Sheria havikinzani kwa namna yoyote na Katiba bali vinakamilisha utekelezaji wa masharti ya Ibara ya 26 (2) na 30 (3) ya Katiba. Ilielezwa kuwa, vifungu hivyo, vinazopingwa havijajaribu kwa namna yoyote ile kurekebisha Katiba kupitia mlango wa nyuma bali vimeweka masharti anwani ya kuzingatia pale mtu anapodai haki yake ya kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 12 mpaka 29 inavunjwa na hapo anapaswa kuwasilisha maombi kwa kuunganisha Ibada cha 26 (2) na 30 (3). Kanuni za kikatiba za mgawanyo wa madaraka; utawala wa sheria na jukumu muhimu la mahakama katika utoaji haki haijaathiriwa na marekebisho yaliyolalamikiwa na zaidi, marekebisho yameweka jukumu katika kuhakikisha utaratibu unafuatwa.

Marekebisho yaliyolalamikiwa yanaendana na matakwa ya Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki; Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa. Aidha, kuhusu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa mhusika kwenye madai ya ukiukwaji badala ya wakuu wa Serikali walioko madarakani, hilo ni takwa la katiba na sheria nyingine za nchi ambapo Mwanasheria Mkuu ndiye Mshauri wa Sheria wa Serikali na mwakilishi wa Serikali katika mashauri yote anayoihusu Serikali.

Baada ya kuchambua hoja za pande zote mbili kwenye Shauri hili, mahakama iliamua kuyatupilia mbali madai ya Bw. Onesmo Olengurumwa. Katika uamuzi huo pamoja na mambo mengine, Mahakama ilieleza kuwa, Misingi ya katiba, ikisimama peke yake inalazimisha kuwa na kanuni za utaratibu kwa ajili ya kuwezesha Mahakama kutathimini kama ombi lolote lililowasilishwa na raia kudai haki ya misingi lina ushahidi. Hivyo, hitaji la kuwa na Hati ya Kiapo chini ya kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu kama ilirekebishwa

mwaka 2020 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 Sheria ya mwaka 2020 ni muhimu sana ili kuunga mkono ombi kwa maana ya kuthibitisha kama ombi lililowasilishwa Mahakamani lina msingi kwa kuzingatia viwango vya kawaida vya haki za binadamu au ombi halikubaliani na kanuni zinazopaswa kuiwezesha Mahakama inayosikiliza shauri kusimamia haki.

Kwa upande mwingine, Kanuni za katiba haziwezi kutekelezwa peke yake bila kuwa na kanuni zinazohusu utaratibu ambazo ni "kanuni ya chujio la malalamiko yanayohusu haki za umma" ambalo takwa la Hati ya Kiapo kinachoeleza namna mwombaji binafsi alivyathorika na kile anacholalamikia ni moja ya chujio linalohitajika chini ya kifungu cha 4(2) cha Sheria kwa ajili ya maombi au mashauri ya haki za umma.

Mahakama ilieleza kwenye uamuzi huu kuwa, hitaji la kuwa na chujiio la malalamiko ya kikatiba linatatumika Kwanza, kuilinda Mahakama ili isishughulike na madai sio tu yaliyokosa msingi wa kisheria bali yasiyo na maslahi ya umma lakini maslahi binafsi na ambayo yamewasilishwa kupitia mwamvuli ya maslahi ya umma. Pili, Mahakama ilisema kuwa, pasipo chujio, itawafanya Waombaji wengi wenye madai yenye hisia ovu kupata uwezekano wa kuwasilisha Malalamiko kwa misingi ya madai ya umma na ambayo siyo halisia na yenye maslahi ya umma. Hivyo, sio rahisi kwa mahakama ya kutambua nia ovu isipokuwa kama kuna hati ya kiapo ya kuunga mkono Ombi hilo. Tatu, Mahakama iliona kuwa, hati ya kiapo kwenye maombi husaidia kuzuia msururu wa kesi ambazo zinaweza kuletwa mahakamani pasipo kuzingatia maslahi ya umma na hivyo, utaratibu uliowekwa na Sheria unatumiwa kusaidia mahakama katika kuthibiti mrundikano wa kesi usio wa lazima.

Nne, Mahakama iliona kuwa, hati ya kiapo ni takwa la Sheria kwa kuwa Mahakama inaposhughulikia kesi ya Katiba inaongozwa na Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu ambapo inatakiwa kutenda haki, ndani ya muda unaofaa na kwa uwiano na kuangalia gharama. Tano, uchujaji wa kesi za madai ya haki za umma kupitia hati ya kiapo itaepusha mahakama kushughulika na mambo ya msingi ndani ya kesi na badala yake itaweza kuondosha kwa haraka mambo mengine ambayo hayana msingi. Mwisho, Mahakama iliona kuwa, kwa kuwa na hati ya Kiapo, itaweza kusaidiwa kupunguza muda na gharama kwa wadaawa.

Mahakama iliafikiana hoja za Serikali kuwa, Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu inaweka utaratibu wa namna ya kusimamia madai ya ukiukwaji wa haki na uhuru chini ya Ibara ya 12-29 ya Katiba na ikisomwa na Ibara ya 26 (2) ya Katiba inayosimamia maombi ya namna hiyo.

Hivyo, kupitia kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu, Mwombaji anatakiwa kupimwa kama ana haki ya msingi anapowasilisha maombi Mahakamani na kuwa ili kugundua hili, lazima kuwe na ukweli katika hati ya kiapo inayobainisha kiwango cha maslahi ya mwombaji kama ushahidi.

Katika hoja nyingine, Mahakama ilikubaliana na hoja za Serikali kuwa kiwango kinachohitajika ili kuthibitisha kesi katika maombi ya ukiukwaji wa haki za msingi chini ya Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu ni kuonyesha kuna kesi ya msingi ya kujibu kwa upande wa Serikali pasipo kuacha mashaka na sio kuweka mazingira ya makisio ya uwezekano wa kuwepo kwa kesi kama ilivyo katika kesi za kawaida za madai.

Mahakama ilijiridhisha kuwa, marekebisho yaliyolalamikiwa yalikusudiwa kuhakikisha uzingatiaji wa taratibu katika kudai haki ya kikatiba na kulinda kanuni ya mgawanyo wa madaraka; utawala wa sheria na jukumu muhimu la mahakama katika utoaji haki na ziko katika kufuata na kuzingatia matakwa ya kimataifa ndani ya Mkataba wa Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki; Mkataba wa Kiafrika kuhusu Binadamu na Haki za Watu na Mkataba wa Kimataifa wa Kiraia na KisiasaHaki.

Kuhusu kufungua shauri dhidi ya Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Spika, Naibu Spika au Jaji Mkuu kwa kitendo au kasoro, Mahakama iliamua kuwa, jukumu la Mwanasheria Mkuu wa Serikali chini ya Katiba, ni Mshauri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu masuala ya sheria, ikimaanisha kwamba, iwapo kuna uamuzi wowote au kutofanya kazi kwa Serikali,Mwanasheria Mkuu anawajibika kwa kitendo hicho na hivyo analazimika kutetea kwa mujibu wa Ibara ya 59(3) na (4) ya Katiba na Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu), [Sura 268 Marejeo ya Mwaka2019].

Mahakama ilizingatia kwa makini mawasilisho ya pande zote mbili juu ya uhitaji kukamilisha nafuu nyingine za kisheria kabla ya kufungua madai ya Kikatiba kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Msingi na Wajibu. Mahakama iliona kuwa, takwa hilo lilikuwepo katika kifungu cha 8(2) hata kabla ya Sheria kurejebishwa.

Mahakama iliona kuwa hata kama kuna ukiukaji wa haki za binadamu, hitaji la kukamilisha hatua za kupata nafuu nyingine za Sheria kabla ya kwenda Mahakamani ni muhimu sana kwa kuwa imejengwa juu ya kanuni kwamba Serikali inapaswa kuwa na taarifa ya ukiukwaji wa haki za binadamu ili kupata fursa kurekebisha ukiukwaji huo kabla ya kushtakiwa mbele ya mahakama.

Katika kesi hiyo, awali, Mahakama ilitamka Kanuni zifuatazo za kuzingatiwa pale mtu anapowasilishwa shauri la Kikatiba Mahakamana Kuu:

**A.** Sheria inapopingwa, Mahakama huwa inalo dhanio kuwa Sheria hiyo ina uhalali kikatiba. Kwa hiyo, Mwombaji anayepinga uhalali huu anahitajika kuanzisha kesi ya msingi juu ya usahihi wa madai juu ya uhalali wa Sheria. Mwombaji ni lazima aoneshe kwa usahihi, kwa kiwango kinachohitajika haki anayodai imekiukwa, namna ilivyokiukwa na nafuu anayotafuta kwa ukiukaji huo. Kwa maneno mengine, kuna dhana ya katiba katika sheria kwamba yule anayedai kuwa Sheria ipo kinyume cha Katiba ajenge hoja kuthibitisha hilo;

**B.** Ili kutathmini na kubaini kama masharti ya Sheria yanayopingwa ni kinyume na katiba, pamoja na mambo mengine vipimo vinne muhimu: Moja, ni kutokuwa wazi. Kama kifungu cha 4 (2); 4 (3); 4 (4), na 4 (5) ya Sheria iliyopingwa vinakinzana na maswala ya msingi ya kisera na ya kibaguzi na yapo kiholela. (ii) Mbili, kama yanatoa haki tofauti kati ya raia. Hapa ni kama vifungu vya 4 (2); 4 (3); 4 (4), na 4 (5) vya vinawatofautisha wananchi kibaguzi. Ikiwa ndio, kama matakwa hayo yanawafanya kutokuwa sawa mbele ya sheria hiyo. (iii) Tatu, ni kama sheria hiyo ina uwiano wowote miongoni mwa watu au kama masharti hayo yanapitiliza matakwa ya Katiba. (iv) Nne, kama vifungu husika vinazingatia haki za binadamu vinavyokusudiwa kwa pamoja na mambo mengine Mkataba wa Afrika wa Binadamu na Haki za Watu na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa.

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

# OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL

**HEAD QUATERS -**
**OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL**
**10 Kivukoni Road**
**P. O. BOX 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Hotline: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Website: www.osg.go.tz**
**Email: info@osg.go.tz**

## POSTAL ADDRESS AND LOCATION OF REGIONAL OFFICES

| | |
|---|---|
| OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 1902, 41218 **DODOMA**<br>Ministry of Legal and Constitutional Affairs - Building (UDOM)<br>Email: dodoma@osg.go.tz | OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 130<br>31101 **MUSOMA**<br>Regional Commissioner's Office Building<br>Email: mara@osg.go.tz |
| OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 1280<br>63114 **MTWARA**<br>Former Mtwara District Council Building<br>Email: mtwara@osg.go.tz | OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 394<br>33101 **MWANZA**<br>Regional Commissioner's Office Building<br>Email: mwanza@osg.go.tz |
| OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 595<br>51108 **IRINGA**<br>Former Iringa District Council Building<br>Email: iringa@osg.go.tz | OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 106<br>35102 **BUKOBA**<br>Ministry of Finance and Planning Building<br>Email: kagera@osg.go.tz |
| OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 564<br>57101 **SONGEA**<br>Regional Commissioner's Office Building<br>Email: ruvuma@osg.go.tz | OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 43<br>37101 **SHINYANGA**<br>Regional Commissioner's Office Building<br>Email: shinyanga@osg.go.tz |
| OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 60<br>21101 **TANGA**<br>Bandari House<br>Email: tanga@osg.go.tz | OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 119<br>45112 **TABORA**<br>Regional Commissioner's Office Building<br>Email: tabora@osg.go.tz |
| OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 202<br>25101 **MOSHI**<br>TRA Building - Moshi<br>Email: kilimanjaro@osg.go.tz | OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 321<br>55103 **SUMBAWANGA**<br>Regional Commissioner's Office Building<br>Email: rukwa@osg.go.tz |
| OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 66<br>23101 **ARUSHA**<br>Regional Commissioner's Office Building<br>Email: arusha@osg.go.tz | OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 710<br>53107 **MBEYA**<br>Madini House<br>Email: mbeya@osg.go.tz |
| OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>P. O. BOX 172<br>47101 **KIGOMA**<br>Kigoma Municipal Council Building<br>Email: kigoma@osg.go.tz | OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL<br>NSSF Commercial Complex, 2nd Floor<br>**MOROGORO**, Plot No. Zone II, Along Old DSM Road within Morogoro Municipality<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |